Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 73 No. 168 | RABI'UL-AWWAL 1433AH | JANUARI 2012 | SULH 1391 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Je! hamwoni ya kwamba Mwenyezi Mungu Aliwatiishieni vilivyomo mbinguni na ardhini, na Akawakamilishieni neema Zake zilizo dhahiri na za siri? Na wako watu wanaobishana katika (mambo ya) Mwenyezi Mungu pasipo elimu wala mwongozo wala Kitabu chenye nuru. ***(Luqman 31:21).***

Kiongozi wa Ahmadiyya duniani awaasa Watanzania:

Msikubali mataifa makubwa kuchota rasilimali zenu



Mh. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Na Jamil Mwanga,

Dar es Salaam

Watanzania wametakiwa kunufaika ipasavyo na matunda ya uhuru walioupata na kujitahidi kutumia raslimali walizopewa kwa ajili ya manufaa yao.

Rai hiyo imetolewa na Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a kupitia salamu zake kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete katika kuadhimisha miaka 50 ya uhuru wa Tanzania bara zilizofikia kilele chake Disemba 9, 2011.

Kiongozi huyo alimweleza Rais Kikwete kuwa nchi zote za Afrika hazina budi kutilia maanani hadithi ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. isemayo: Kiongozi wa nchi ni mtumishi wa Taifa.

Endelea uk. 3



Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a

Makhalifa Waongofu, Hadhrat Imam Hussein r.a. wote walikuwa Wachamungu

Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. (Kiongozi wa Ahmadiyya duniani) katika moja ya hotuba zake za Ijumaa hivi karibuni alizungumzia juu ya utakatifu na utawa wa Makhalifa waongofu na Masahaba wengine wa Mtukufu Mtume s.a.w. akiwemo Imam Hussein r.a.

Akimnukuu Masihi Aliyeahidiwa a.s., katika hotuba hiyo alisema:-

Masihi Aliyeahidiwa anasema ya kwamba hawa wote walikuwa ni wacha Mungu ambao walijitolea maisha yao kwa Mwenyezi Mungu na kwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) na walikuwa na huruma kubwa sana kwa binadamu. Kiongozi huyo wa waaminio alisema ya kwamba kufuata nyayo za Makhalifa waliongozwa "Khulafat-ur-Rashidin"

Endelea uk. 2

Tafsiri yetu ya Qur'an Tukufu 'Mama wa Kiswahili'

Na Mahamood Hamsini Mubiru, Dar es Salaam

Wazungupule wa ushairi nchini mwetu. Wametuachia utamaduni wa kupendana bila ya kujali itikadi, unakotoka na wala dini yako. Usuhuba baina ya Mathias Mnyampala na Sheikh Kaluta Amri Abedi umezaa kitabu: *Historia ya maisha ya marehemu Sheikh Kaluta Amri Abedi*. Usuhuba wa Shaabani Gonga wa Dar es Salaam na Khamis Amani KhamisNyamaumewaDodoma



Mahmud Hamsini Mubiru

ndiyo ulizaa kitabu *Diwani ya Nyamaume* iliyokusanya na sahibu wake Shaabani Gonga. Usuhuba mwingine wa kuvutia ulikuwa baina ya Sheikh Kaluta Amri Abedi na Sheikh Shaabani Robert wa Tanga. Usuhuba huo ulikuwa bayana zaidi wakati wa malumbano yale maarufu, wakati Shaabani Robert alipotunga shairi lake lenye kibwagizo *ndoa mbaya afadhali kuliko ujane mwema*. Shaabani Robert alishambuliwa darmadar. Lakini katika tufani

Endelea uk. 3

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Makhalifa Waongofu, Hadhrat Imam Hussein r.a. wote walikuwa Wachamungu

Kutoka uk. 3

ndio kilele cha ufaulu kwa mwaminio kwa sababu watu hawa walimpenda sana Mwenyezi Mungu na walikuwa tayari kutoa maisha yao kwa ajili ya kumtumikia Mtukufu Mtume Muhammad (saw).

Hadhrat Abubakar (ra) alikuwa ni mwema sana mwenye mapenzi makubwa na uso wake uling'aa kwa miale ya kiucha Mungu na mapenzi yake kwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) yalikuwa ni ya kupigiwa mfano.

Kumhusu Hadhrat Umar (ra) Masihi Aliyeahidiwa anasema Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alisema ya kwamba "Shetani mwenyewe anaogopa kivuli cha Umar" na aliendelea kusema ya kwamba kama angekuwepo mtume baada yake, angekuwa Umar (ra). Pia aliendelea kusema ya kwamba; "Walikuwepo Muhadithina katika dini zilizopita, na katika umma huu Muhadithina ni Umar".

Masihi Aliyeahidiwa alisema ya kwamba Mwenyezi Mungu Amenifanya nielewe ya kwamba Hadhrat Abubakar, Umar na Othuman radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yao, walikuwa na utii wa hali ya juu na walikuwa wameongozwa. Ni miongoni mwa wale ambao Mwenyezi Mungu Amewamiminia mapenzi yake.

Masihi Alieyahidiwa anasema ya kwamba; "Hadhrat Ali (ra) alikuwa mcha Mungu sana na alikuwa miongoni mwa wale ambao Mwenyezi Mungu Anawapenda sana" Yeye alitokana na ukoo wenye heshima na alikuwa kiongozi wa watu wake. Alikuwa ni simba wa Mwenyezi Mungu. Alikuwa ni mkarimu na mwenye moyo ulio safi na mapambano ya vita yalionesha ushujaa wake. Alikuwa anazungumza kwa sauti ndogo lakini mwenye ufasaha wa hali ya juu.

Akizungumzia juu ya Masahaba wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw), Masihi aliyeahidiwa anasema; "Walipewa fungu kubwa la imani kiasi hiki ya kwamba maadui wao wa kidunia licha ya nguvu zao zote na hila, walishindwa kuwaangamiza".

Khalifa Mtukufu alisema ya kwamba Masihi Aliyeahidiwa alisema ya kwamba aliwapenda Masahaba wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) na kizazi chake kwa sababu ya kujinasibisha na Mtukufu Mtume (saw). Khalifa Mtukufu alisema ya kwamba kuwaheshimu wazee wetu ni sehemu ya imani, lakini wakati huo huo lazima tumpe kila mtu haki yake. Ama sivyo tutakuwa tunatenda dhambi. Alisema ninampenda Ali (ra) na wanae wawili na adui yao ni adui yangu. Hussein alikuwa ni mcha Mungu sana na alikuwa miongoni mwa wale ambao wametakaswa na Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yake. Hapana shaka yeye ni miongoni mwa walioteuliwa huko peponi. Mtu yeyote anayeonyesha husuda hata ndogo kiasi gani -aelewe ya kwamba anaondoka katika imani. Ucha Mungu wake na mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu, uvumilivu hayo yote ni mfano kwetu sisi.

Khalifa Mtukufu alimaliza kwa kusema ya kwamba, haya ndiyo mafunzo mazuri yaliyoletwa na Masihi Aliyeahidiwa. Mafundisho yanayowaleta watu wote pamoja na kujenga mapenzi na kuhurumiana.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu awajaalie binadamu waweze kuelewa ujumbe huu ulioletwa na Masihi Aliyeahidiwa ili waache kuuwana.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Wasifu wa Mwalimu Majid Sudi Namwete (1967 - 2011)

Na Mwalimu Mohamedi Namwete - Dar es Salaam

Allah Mwenye adhama, kama ilivyo kawaida Aliifanya siku ya Jumatano ya mwezi wa kumi na moja ya tarehe ishirini na tatu mwaka wa elfu mbili na kumi na moja, ilikuwa saa nne na nusu asubuhi, ni hapa jijini Dar es Salaam alipoifanya ni ya huzuni na majonzi yaliyozagaa sio tu hapa Dar es salaam bali nchi nzima.

Ilikuwa ni pata shika, pale mitandao ya mawasiliano yote ilipopata wakati mgumu, wakati wa kutangaza kwa ghafla kifo cha Mwalimu wetu mpenzi, Mwalimu Majid Ahmad Sudi - maarufu kwa jina la ushairi 'Simba dume'. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea.

Ukweli wa haya ulithibitika siku iliyofuata, siku ya Alhamisi, tarehe 24/11/2011, saa 11 jioni katika viwanja vya makaburi ya Waahmadiyya Wailes Temeke Dar es salaam ambavyo, vilifurika umati mkubwa wa watu.

Mimi sikuamini macho yangu, maana wakati huo nilikuwa mmoja wa walioingia wakati huo, tukitokea Muhimbili hospitali ambako mwili wa marehemu ulihifadhiwa na kulazimika tuombe rasmi, kuosha, kuuvisha sanda - tayari kwa mazishi. Tukiwa katika msafara mrefu wa magari yaliyousindikiza mwili wa marehemu yakiongozwa na mapikipiki ya akina Bw. Bumbo na kufuata gari la Bw. Amir Abedi Kaluta huku gari la Jamaat lenye maandishi ya "Ahmadiyya" nyuma pia pick-up nyingine iliyobeba mwili wa marehemu na msafara huo mrefu uliingia makaburini na kuongeza idadi ya magari yaliyojaa kama utitiri. Kwa neno zima hali ile ilionekana kama kwamba watu wa Dar es salaam na magari yao siku ile ni kama waliacha mambo yao yote na kushughulika na mazishi ya Mwl. Majid tu, au simba dume kwa lakabu yake ya kishairi.

Hali hiyo ilitokea kwa nini?

Bila shaka yeyote hali hiyo ilitokea kwa sababu ya hali halisi ya marehemu Mwl. Majid Ahmad Sudi Namwete, kuwa maarufu kwa kuwa ni mchapa kazi, tena aliye makini, muhubiri mahiri, mtunzi wa makala, na mtoa mada mashuhuri za mvuto, pia ni msomaji fasaha. Alikuwa mtunga mashairi Simba dume mkereketwa. Pia mcheshi mwenye kutoa ushauri, aliye na msimamo thabiti.

Bila shaka kwa hali yake hiyo na mengine mengi, ambayo kila aliyepata nafasi ya kuishi au kuwa karibu nae kwa muda mfupi tu atakuwa shahidi wa haya nisemayo, au zaidi. Na hasa kwa vile marehemu, alipata nafasi ya kuishi na kufanya kazi mikoa mbalimbali na hata nje ya nchi pia - huko Malawi, ambako alirudia zaidi ya mara mbili. Askari huyu makini wa Masihi Aliyeahidiwa (as) amefariki katika Jeshi lake akiendelea kutimiza majukumu yake, huko mkoani Iringa ambako ugonjwa uliopelekea kifo chake ulikomuanzia hatimaye kuhamishiwa Hospitali ya taifa

ya Muhimbili, ambako umauti ulimfikia.

Kuzaliwa:

Mwl. Majid Ahmad Sudi Namwete alizaliwa tarehe 06/09/1967, katika kijiji cha Mndumbwe kata ya Mdimba Sudi, tarafa ya Mahuta, Wilaya ya Tandahimba mkoa wa Mtwara.

Yeye katika watoto wa Marehemu Mzee Ahmad Sudi Namwete ni mtoto wa tano, kati ya watoto 11. Kati yao wa kike ni watatu (3) na wa kiume ni wanane (8), mwandishi wa makala hii - ni wa tatu kuzaliwa.

Shule ya Msingi na Sekondari

Mwalimu Majid Sudi, alipata elimu yake ya Msingi katika shule ya Msingi Mndumbwe, kijijini hapo na kupata cheti mwaka 1983. Hapa pia ni vizuri ikumbukwe kuwa alipata kusoma elimu ya Sekondari akiwa kazini na kufanikiwa kupata cheti cha form IV (O-level) katika miaka ya tisini. Elimu hii aliisoma kwa mtindo ule ujulikanao kama "Elimu kwa njia ya Posta", kwa muda wa miaka miwili.

Vuguvugu la mahubiri ya Kiahmadiyya - Kanda ya Kusini:

Wakati Mwalimu Majid A. S. Namwete anamaliza shule ya msingi miaka ile ya mwanzo ya themanini, kulikuwa na joto kali katika kanda ile ya kusini ya mahubiri ya Jamaat Ahmadiyya. Jitihada za makusudi za mahubiri yaliyochanganyika na maombi ya Waahmadiyya wote duniani yakiongozwa na Khalifatul Masih. Askari hao wa Masihi Aliyeahidiwa wakiwa wamesambaa sehemu nyingi, walifanikiwa kuinasa familia ya marehemu Mzee Ahmad Sudi Namwete.

Kwa mfano zama hizo timu ilikuwa hivi - Makao Makuu Amir na Mbashiri Mkuu alikuwa ni Maulana Sheikh Abdulwahab sahib, pale Newala alikuwepo Mwalimu Hassan Athumani Mrope sahib, Newala mjini pia walikuwepo akina Mzee Abdullah, Mwalimu Seif Hassan Nakuchima - Mmeda, Mzee Ismail Mpukutile - Lindi Mjini, Nahadullah Matolla - Masasi, Suleiman Jeilani - Mahuta, Hamisi Bin Mshamu - Nyangamara, akina Mwalimu Sabbihi Mtima - dinembo wakishirikiana na akina Mwalimu Uledi,, Mshamu Rashidi Mtepa, Mzee Nanyou, akina Yusufu bin Mmoto - Nachingwea, hawa na wengine katika kanda ile walihusika katika namna moja au nyingine kufanikisha zoezi hilo hususan katika siku zile.

Kutokana na vuguvugu hilo, Allah Karimu kama ilivyo kawaida yake kupokea jitihada za wafanya jitihada kusema kweli, kwa maombi yao ya usiku na mchana, aliiwezesha pia familia hii kujiunga na Jumuiyya hii tukufu ya Masihi Aliyeahidiwa (as) tarehe27/05/1983, Mzee Namwete mwenyewe na baada ya siku chache familia yake akiwemo marehemu Mwalimu Majid Sudi, na baadhi ya watoto, waliokuwa wadogo kwa wakati huo.

Wimbi hilo, sio tu kwamba lilimkumba marehemu na familia yake tu, bali kujiunga tu kwa Mzee Namwete na familia yake ikawa Jamaat imeongezewa nguvu ya ziada katika kanda hiyo, ndipo kutokana na Mzee Namwete nae ambaye alikuwa mahiri katika uwanja wa hoja kukasababisha kupatikana Jamaat zingine za jirani na Mdimba kama vile Mndumbwe, Mivanga, Tandahimba, Nahmnyanga n.k

Endelea uk. 4

Tafsiri ya Qur'an Tukufu 'Mama wa Kiswahili'

Kutoka uk. 1

hiyo Sheikh Amri Abedi aliwaambia 'na watakaokuroga na Robert harogeki'. Akifurahia shime na msaada huo kutoka kwa Sheikh Kaluta Amri Abedi, alifurahi na kuimba.

Heko Amri Abedi, mwenye fadhila na utu
Heko ukidhi mradi, usitawi kati yetu
Heko kijana asadi, katika biladi zetu.
Shaabani Robert alipata faraja kubwa sana kuwa pamoja na Sheikh Amri Abedi na alikuwa na uhakika kwamba akiwa na Sheikh Amri, ushindi bila shaka utakuwa wao. Akisisitizia hilo aliimba.

K. Amri Abedi, akhsante sana mgosi
Kushikwa we na madadi, nilijua haikosi
Nami ninajitahidi, kuomba kwa luqudusi
Msimbe na Ibilisi, takosaje kudarana?
Tukipigana wawili, kaskazi hata kusi
Zije kwa dhoruba kali, kutufuata sisi
Twaweza kuzikabili, pasi na wasiwasi.

Hivyo mwaka 1962 wakati Sheikh Kaluta Amri Abedi ni Mkuu wa Mkoa wa Tabora. Mwalimu Abdallah Ali Ng'ambage, Mbashiri wa Jumuiya ya Ahmadiyya aliyezaliwa huko Kilwa mwaka 1939. Alipewa uhamisho wa kuwa Mbashiri wa Ahmadiyya mjini Tanga. Kabla hajaondoka, Sheikh Kaluta alimpa salamu mahsusi amfikishie Sheikh Shaaban Robert na ajitambulishe kwake. Mwalimu Ng'ambage alipofika Tanga alionana na Sheikh Shaaban Robert. Alimweleza Sheikh Shaaban Robert kuwa yeye ni mwanafunzi wa Sheikh Kaluta Amri Abedi, alifurahi sana. Huku akitabasamu alimwambia Mwalimu Ng'ambage kuwa hapa ni nyumbani kwako.

Shaaban Robert aliishi barabara ya saba, ambapo alikuwa na duka la vitabu. Kazi hii ya kuuza vitabu ilifanywa na mkewe. Shaaban Robert alimweleza Mwalimu Ng'ambage aweke vitabu vya Jumuiya katika duka lake.

Mazoea baina ya Mwalimu Ng'ambage na Shaaban Robert yalikuwa makubwa wakawa wanatembea pamoja katika mitaa ya Tanga. Watu wengi mjini hapo walikuwa wameamini kuwa Shaaban Robert alikuwa amejiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya. Lakini ukweli ni kwamba hakuwa amejiunga isipokuwa alikuwa ni mpenzi tu na ambaye alikuwa anaendelea kusoma vitabu vya Jumuiya. Watu wa Tanga walipozidi kumsakama na kusema yeye ni Mirzai kwa njia ya hekima alisema.

Nashikilia ukale, ambapo hapana budi
Na huacha vilevile, iwapo haunifidi
Nitabadili milele, siwezi kuwa abidi
Wa kutenda yaleyale, kuizuia juhudi.

Kutokana na mazoea hayo ya kutembea pamoja, kila Sheikh Shaabani Robert alipopata shughuli ya kijamii alimkaribisha Mwalimu Ng'ambage. Waliwahi kwenda pamoja, shule ya Magira Middle School ili kuzungumza na wanafunzi wa Kiislam waliokuwepo shuleni hapo. Tukio kubwa lililotokea miezi michache kabla ya kifo chake. Ulifanyika mjini Tanga mkutano wa Kamati ya Lugha ya Kiswahili chini ya Uenyekiti wa Shaabani Robert. Mkutano huo ulifanyika Tangamano na wajumbe wa ndani na nje ya nchi walihudhuria. Wajumbe wapenzi wa Kiswahili walitoka Unguja, Kenya, Uganda, Afrika ya Kusini, Zambia, na Malawi. Mazungumzo yalikuwa ni ya kuendeleza lugha ya Kiswahili. Katika mazungumzo Mwenyekiti alitoa shukrani kwa taasisi na watu binafsi kwa mchango wao wa kuendeleza Kiswahili. Na alisifu sana mchango wa Jumuiya ya Ahmadiyya hususan Tafsiri ya Qur'an Tukufu iliyotafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Mubarak Ahmad na kuchapwa mwaka 1953. Shaabani Robert alisifia uzuri wa Kiswahili katika tafsiri na kuweka bayana kuwa Tafsiri hiyo ni mama wa Kiswahili. Kauli hiyo iliamsha hisia kali kutoka kwa baadhi ya wajumbe ambao walipinga kabisa wazo hilo la kuiita Tafsiri hiyo ya Ahmadiyya kuwa ni mama wa Kiswahili.

Wa kwanza kusimama kupinga kauli hiyo ya Mwenyekiti alikuwa ni Bw. Suchak, Mtanganyika mwenye asili ya India, mfanyabiashara maarufu mjini Tanga. Yeye alisimama na kusema, ndugu wajumbe aliyetafsiri Qur'an Tukufu ni Mpanjabi toka Pakistan, hivyo Kiswahili hakijui. Hivyo Tafsiri hiyo haiwezi kuwa Mama wa Kiswahili. Mwenyekiti Shaabani Robert alimjibu, tumesikia maoni yako mjumbe na tunayaheshimu, na tunalolifahamu ni kwamba, wewe ulikuja hapa Tanganyika kuuza bizari na pilipili sokoni na si mtaalamu wa Kiswahili na wala hukuja kujifunza Kiswahili. Mhindi wa watu alipigwa na butwaa, akanywea na asiwe na lolote la kujibu.

Wa pili kusimama kupinga hoja ya Mwenyekiti, ni Waziri wa Elimu wa Unguja, kwa mbwembe na makeke ya kujiamini alisimama na kusema, katu hatuwezi kuifanya Tafsiri hiyo kuwa Mama wa Kiswahili, kwa sababu msomi maarufu wa dini ya Kiislam Afrika ya Mashariki, Sheikh Abdullah Saleh Farsy yumo mbioni kutafsiri Qur'an Tukufu katika Kiswahili na mwaka 1967 itakuwa imetoka na hii ndiyo itakayoweza kuitwa Mama wa Kiswahili. Mwandishi yule maarufu wa *Kusadikika, Kufikirika, Adili na nduguze, Utu bora mkulima* na mashairi lukuki alisimama na kumwaga falsafa. Kwa sauti imara alisema, wajumbe baba gani mjinga na mpumbavu wa kiasi gani watoto wake wanalia njaa na unga wa uji upo halafu anawaambia watoto hao waache kulia njaa wangoje pilau itakayopikwa baada ya miaka saba. Wajumbe wote waliangua kicheko. Kijana huyo wa Unguja akatokwa na jasho jembamba ingawaje ilikuwa wakati wa kipupwe. Akashika kiganja chake kuficha uso wake na akaomba ardhi ipasuke ili angalau aepukane na zahama ambayo alikuwa amekumbana nayo.

Kwa maelezo haya, Mwenyekiti hakuamini ya kuwa yupo mwingine atakaediriki kujenga hoja. Lakini binadamu tunatofautiana mithili ya vidole kwenye viganja. Alisimama Mkuu wa Wilaya ya Tanga, yeye akaona fupa lililomshinda fisi labda yeye angeliliweza. Yeye alisema, mimi nakubali Tafsiri hiyo isiwe Mama wa Kiswahili, Kwa sababu Rafiki yake Sheikh Alli wa Tanga ameshatunga kitabu cha kupinga kitabu hiki. Kwa mara nyingine tena Mwenyekiti aliwajibika kusimama na kutema cheche. Nasikitika tena nasikitika sana, DC mzungu kukosa aibu, Sheikh Alli unasema alikuwa rafiki yako? Urafiki wa kufungana jela urafiki gani huo? Si wewe uliemtia pingu? Je Mapadre wangapi umewatia jela? Nionyeshe ukurasa wa kitabu cha Sheikh Alli alipozungumzia Kiswahili. Mimi nilisahihisha kitabu chake na nilichoona mimi humo ni mambo ya dini. Mzungu wa watu alishikwa na kigugumizi cha ghafla na asiwe na la kusema. Akaloa kama kondoo aliyenyeshewa na mvua. Ni mtu tu aliyekuwa karibu nae aliyemkumbusha kiti chake kilikuwa wapi.

Hakuna mwingine aliyesimama kusema lolote na kikao hicho kikatengeneza historia kwa kukubali kwa sauti moja kuwa Tafsiri ya Qur'an Tukufu kwa Kiswahili ya Jumuiya ya Ahmadiyya iliyotolewa mwaka 1953 ndiyo Mama wa Kiswahili.

Mwisho.

Msikubali mataifa makubwa kuchota rasilimali zenu

Kutoka uk. 1

Aidha, alisema ili uhuru huu ambao umepatikana baada ya kipindi kirefu cha ukoloni na utumwa uweze kudumu, Sheria zinazotungwa katika nchi zinatakiwa ziwe sawa kwa maskini na matajiri. Alitahadharisha kuwa vyinginevyo, mataifa yenye nguvu yatawaghilibu kwa lengo la kuzichota rasilimali zenu.

"Lakini endapo hamtalifuata hili, mataifa makubwa kwa mara nyingine tena yataingia katika nchi zenu na kuchukuwa malighafi zenu kupitia mipango ya udanganyifu na hila ama kwa sababu zozote ziwazo zisizo na ukweli ndani yake", alisema.

Alisema, ili taifa liweze kupata maendeleo, viongozi wa nchi zinazoendelea wanatakiwa kutimiza haki za watu wao na pia watu wenyewe watoe kipaumbele kwa maslahi ya taifa lao. Aliongeza kusema kuwa kama nchi zote za Afrika zitazingatia jambo hili, bara hilo litapiga hatua kimaendeleo, tena kwa kasi kubwa.

"Nina uhakika kabisa kwamba, kama nchi za Kiafrika na watu wake wataungana na kutimiza yale yote yanayotakiwa na adili basi siku moja bara la Afrika litaibuka kuwa taifa lenye nguvu duniani. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awezeshe hilo. Inshallah".

Katika salamu hizo, Khalifa Mtukufu a.t.b.a alirejea fundisho la Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. kuhusu mtu kuipenda na kuwa mtiifu katika nchi anayoishi. Kwa hakika utiifu kwa nchi ni msingi madhubuti wa Muislam. Hivyo, Waislamu Waahmadiya katika nchi yoyote wanapoishi wanatakiwa siku zote kufanya jitihada katika kuleta maendeleo ya nchi zao na kuwatumikia wananchi kwa kadri ya uwezo wao.

Aidha, Kiongozi huyo wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya alimhakikishia rais Kikwete kuwa Jumuiya hiyo daima itaendelea kutoa huduma kwa Tanzania, wakati wowote itakapohitajika, huduma ambayo itakuwa kwa manufaa ya wananchi wote wa Tanzania.

Alisema, Jumuiya Ahmadiyya itatoa huduma hizo sio kama hisani au kupata malipo bali kwa shauku moja tu ya kuwatumikia binadamu. Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, Waahmadiyya Waafrika wazalendo ambao hali zao kidogo ni nzuri hutumia mali zao ili kuwasaidia wananchi wenzao bila kujali dini na hii ni kupitia miradi inayosimamiwa na Jumuiya hiyo. Alisema miradi mingi ya kijamii imo katika nchi za Afrika ikiwemo Tanzania.

Akifafanua kuhusiana na miradi hiyo, Khalifa Mtukufu a.t.b.a alisema kuwa kwa miaka 8 ama 9 hivi Jumuiya Ahmadiyya imejitahidi sio tu kuwafanya waafrika wawe karibu na Mwenyezi Mungu bali pia kuwakumbusha juu ya wajibu wao mkubwa kwa bara lao.

Akizungumzia kuhusu historia ya Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya nchini Tanzania na mchango wake katika harakati za uhuru, Khalifa Mtukufu a.t.b.a alimweleza Rais Kikwete kuwa Jumuiya Ahmadiyya ilisajiliwa nchini Tanzania na pia katika nchi nyingi za Afrika kabla ya uhuru kupatikana. Alitoa mfano wa nchi ya Sierra-Leone kuwa viongozi wa nchi hiyo walikiri jinsi Jumuiya Ahmadiyya ilivyosaidia nchi hiyo kujipatia uhuru, pamoja na huduma za kijamii zinazotolewa na jumuiya Ahmadiyya. Kwa upande wa uhuru wa Tanzania, Jumuiya Ahmadiyya ilitoa mchango adhimu na usioweza kusahaulika. Miongoni mwa waliochangia ni Sheikh Amri Abedi ambaye alipata mafunzo ya kuwa mbashiri wa dini kwenye Makao Makuu ya Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya, Rabwah, Pakistan. Shekh Amri Abedi ambaye alichaguliwa kuwa Meya wa kwanza wa mji wa Dar es Salaam na ambaye pia alichaguliwa kuwa Mbunge wa LEGCO baada ya kupata ushindi wa kishindo, mara kwa mara viongozi wa nchi walikuwa wakishauriana naye na kunufaika na hekima zake.

Vile vile, Mwaka 1963 aliteuliwa kuwa Waziri wa Sheria. Alipendwa na kuheshimiwa katika wajibu wake huu na hivi leo anakumbukwa kwa huduma yake kubwa kwa taifa lake.

Halikadhalika, Khalifa Mtukufu a.t.b.a alisema Mfano mwingine wa huduma ya Jumuiya ya Ahmadiyya kwa Taifa ni kijana mzalendo wa Kiahmadiyya mwenye asili ya kiasia aliyebuni jina Tanzania.

Mwishoni Khalifa Mtukufu a.t.b.a alimwomba Mwenyezi Mungu Ambariki Rais Kikwete na watanzania na Awawezeshe kupata maendeleo makubwa kama taifa katika hali ya amani, upendo na utulivu.

Wasifu wa Mwalimu Majid Sudi Namwete

Kutoka uk. 4

Mwalimu mwenyewe anasimulia jinsi alivyojiunga. Ilikuwa usiku wa siku hiyo (Eid-il-Fitri 1983) ndiyo ikawa ile siku, iliyosubiriwa kwa hamu kubwa na familia ya marehemu Mzee Ahmad Sudi Namwete, Bi. Fatma binti Aheleke Nayopa, na watoto waliokuwepo hapo nyumbani kipindi hicho ambao ni Majid A.Sudi, Sudi A. Sudi, Rajab A. Sudi (marehemu), Hamza A. Sudi (marehemu), Jamil A. Sudi na dada yake Bi. Rehema A. Sudi.

Wasuni wakafanya maandamano makubwa sana, siku hiyo ya Idi-il-fitiri ya mwaka 1983. Masheikh wakubwa wa kijijini hapo Mdimba waliokuwa hapo kabla, wakihitilafiana - walikubaliana na kuwa kitu kimoja na wakatoa fat'wa ya "ukafiri" kwa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya na kutangaza vikwazo dhidi ya marehemu Mzee Ahmad Sudi Namwete na familia yake, kwamba "akifa tusimzike", "Akiumwa tusimjulie hali, wala na yeye asitujulie hali". Vikwazo vilikuwa vingi, hususan katika mambo ya kijamii. Mwisho, hata sisi watoto wa marehemu ambao tulikuwa tunasoma madrasa moja hapo kijijini, Mudir wa madrasa hiyo (ambaye sasa ni Sheikh wa Bakwata mkoani Mtwara) alitusimamisha, bali alituondoa kabisa chuoni kwake kwa ujumla matokeo ya fat'wa hizo yalitaka kuleta madhara kwa familia yetu, kama siyo msaada maalum wa kimbingu. Kwa mfano watoto wa marehemu walipata kutendewa yafuatayo:- mmoja alichomwa kisu (Hamza), hata Sudi naye alitendwa tendo hilo hilo, naye Rajabu akafukiwa shimoni mzima mzima (tunamshukuru Allah kuwa hali hiyo haikuleta madhara makubwa) hali ya mambo hivi sasa ni tofauti sana.



Maulana Sheikh Abdulwahab Ahmad sahib (kulia) ambaye alimshawishi baba mzazi wa Mwl. Majid ili amtoe waqfu kijana wake akiwa kwenye picha ya pamoja na mzee Muhammad Manoro wakati alipomtembelea nyumbani kwake mjini London mwaka 2008

Alivyotolewa Waqf

Jinsi alivyotolewa Waqfu pia yeye mwenyewe Mwalimu Majid anasema kuwa; ilikuwa ni kutokana na Mkutano wa mwaka Jalsa salana ya mikoa miwili - Lindi na Mtwara kufanyika Mdimba - kijijini hapo Disemba 1983. Mkutano huo ambao ulihudhuriwa na Maulana Sheikh Abdulwahab Ahmad sahib, baada ya mkutano huo Maulana aliacha gumzo kubwa Mdimba. Mbali na kuasa askari wa kwanza wa Imam Mahdi wa kutoka nje ya Afrika, pia tabia yake njema ya Kisahaba aliyoionyesha ilimuweka katika chati za juu miongoni mwa watu wema kwani hakujali aina gani ya chakula, wala malazi. Aliishi kama mwenyeji wa Mdimba. Baada ya siku tatu (3) za mkutano, Mwanazuoni huyo alimshauri baba (Mzee Namwete) kuwa amtoe mwanaye mmoja Waqf kati ya wanawe wawili waliokuwa wanamaliza elimu ya msingi wakati huo yaani Majid Ahmad Sudi au Sudi Ahmad Sudi.

Baada ya tafakuri ndefu, marehemu Mzee Namwete alifikia muafaka na aliamua kumtoa kijana wake Majid. Hatimaye kijana huyu alipelekwa Jamia Ahmadiyya Morogoro na baada ya kuhitimu masomo yake akaitumikia Jamaat akiwa Mwalimu wa Jamaat katika mikoa mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi.

Newala Mission

Hivyo basi baada ya ushauri huo, na tafakuri hiyo, iliyofikiwa muafaka huo ulimfikisha marehemu Mzee Ahmad Sudi Namwete (Mungu Amuweke mahali pema), kumkabidhi Mwalimu Majid Sudi moja kwa moja pale "Newala Ahmadiyya Muslim Mission", wakati huo pale alikuwepo Mwalimu mzoefu na mahiri wa siku nyingi ambaye ni Mwalimu Hassan Athumani Mrope ambaye alimpokea kwa mahaba na kwa moyo mkunjufu. Hivyo Mwalimu Majid alianza masomo yake rasmi ya dini ya miaka mitatu (3) kuanzia 1984 hadi 1986.

Bila shaka yeyote, alionekana kuwa na uwezo mkubwa wa kuyamudu masomo yake, bali majaribio na mitihani alifuzu vizuri. Hali hiyo kwa uwezo wa Allah Karimu ilimuwezesha kustahili kujiunga na masomo ya juu yanayotolewa na chuo chetu cha Jamia kule Morogoro.

Tahir Missionary Training College - Morogoro:

Mwalimu Majid Sudi, akiwa chuoni hapo alifanikiwa kusoma na kuhitimu vizuri masomo yake ya ubashiri kuanzia mwaka 1987 - 1990.

Nakumbuka wakati huo mimi nilikuwa naishi hapa Dar es salaam, hivyo kuwepo kwake chuoni Morogoro kuliniongezea jukumu kwa kiasi fulani kuhakikisha kuwa sio tu kumuwezesha upande wa sabuni, bali kumjenga kisaikolojia ili lengo na shabaha lifikiwe. Alhamdulillah Mwenyezi Mungu Alituwezesha kutekeleza majukumu hayo na Mwalimu alihitimu masomo yake vizuri.

Kuanza kazi na kuoa:

Mwalimu Majid Ahmad Sudi Namwete alimaliza masomo na kuhitimu vyema na kupata shahada ya Ualimu mwaka 1990. Ndipo kwa msaada wa Allah Karimu Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya yenyewe iliamua kumpa kazi rasmi ya ualimu, ubashiri ndani ya Jamaat. Hivyo iliamua aanze kazi mkoani Tanga. Tarehe 23/10/1990 akiwa kama "Mbashiri wa Mkoa -Tanga". Baada ya kuanza kazi, ili afanye kazi zake kwa utulivu na bila mkanganyiko wa mawazo, Mwalimu aliamua kufanya nikah - ndoa mwaka uliofuata yaani 1991. Alimuoa Bi. Amina binti Seif Hassan Nakuchima wa Mmeda, Tandahimba - Mtwara.

Hapa niseme Mwalimu Majid Sudi kwa kweli alikuwa mchapa kazi, ndiyo maana kutokana na uwezo wake bali kipaji chake maalum alichokuwa nacho, akaweza kufanya kazi vizuri Tanga. Tanga ni kati ya sehemu chache hapa nchini ambazo kimahubiri zinataka lazima uwe mahiri wa fani hiyo. Kwa msaada wa Allah Karimu kama zilivyo sehemu nyingine chache hapa nchini Mwalimu kwa ushahidi wa wa-Tanga wenyewe na baadhi ya waliokuwepo huko siku hizo, wanakiri kuwa kilikuwa kipindi cha aina yake. Watu kama akina Mzee Abbasi Mketi, Mzee Bakari Ng'anzi (marehemu), Mzee Tupa, akina Amran Duage (marehemu) na wengine wengi, endapo ungepata nafasi ya kukutana nao wana mengi juu ya zama hizo.

Alifanya kazi sehemu mbalimbali hadi nchini Malawi:

Kwa msaada wa Allah Karimu, Mwalimu Majid Sudi alipata kufanya kazi sehemu mbalimbai hapa nchini hadi nchi ya jirani -Malawi huko Lilongwe na vitongoji vyake.

Kama inavyoeleweka wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa (as) ndio wataalamu wa Qurani Tukufu na vitabu vingine vya dini, ikiwemo Biblia, bali ndio waanzilishi wa kuvisuluhisha vitabu hivyo na dini hizo kwa fani hizo zilimwezesha Mwalimu Majid Sudi kuhamishwa kutoka mkoa huu hadi mwingine katika zama zake za uhai wake kikazi.

Nakumbuka baada ya kufanya kazi kwa mafanikio mkoani Tanga Mwalimu alihamishiwa Ifakara - Morogoro na baadae Kilangalanga - Songea, baada ya hapo aliletwa Morogoro mjini kusimamia Hospitali ya Jamaat pale na baadae akapelekwa mkoani Arusha ambako alisimamia mikoa miwili yaani Arusha na Kilimanjaro, alipohamishwa hapo alipelekwa tena mkoani Morogoro akiwa Mwalimu wa chuo cha Tahilr Missionary College. Baada ya kuwanoa vijana hapo, kama alivyosema yeye mwenyewe akiwa na jopo la walimu wenzake mmojawapo aliyekuwa nae sambamba ni Mwalimu Juneid, hata walipohama walihamishwa kwa mpigo yeye Juneid akielekea Urambo- Tabora na Mwalimu Majid Sudi alielekea Milima ya mkoani Iringa.

Mwalimu akiwa mkoani Iringa amepata mara mbili kutumwa na Jamaat kufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (as) huko Malawi, ameifanya kazi hiyo kwa mafanikio makubwa, alisaidiana na Mwalimu makini - mwalimu Stambuli, ambaye pamoja na kuwa yupo nchi ingine hupatikana Dar, kama wapatikanavyo walimu wa humu humu nchini. Huyu ndiye hasa aliyepata nafasi ya kumuonyesha Mwalimu Majid Sudi siyo tu staili, bali mikoba ya namna gani ya kuishi, kukaa,, kuwasoma, na mengine, watu wa kule na mazingira yao. Nakumbuka aliporudi kule mara ya mwisho, Mwalimu alitoa makala ihusuyo nchi ya Malawi na mazingira yake - akieleza jinsi alivyofikisha ujumbe wa Masihi aliyeahidiwa (as) ndani ya gazeti letu la Mapenzi ya Mungu.

Uwezo wa kazi:

Mwalimu Majid Sudi ukweli uhusuo uwezo wake wa kazi, pamoja na yote hayo yaliyotangulia kwangu nisingeyapa uzito wa kuyaeleza kadamnasi, bali nimehakikisha hilo mimi mwenyewe, wakati ule nilipopata nafasi ya kuonana na Maulana Sheikh Amir na Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir sahib, nikiwa na katibu mwenza wa Jamaat Tanzania tulipofika ofisini kwake kumpa taarifa ya ugonjwa, bali maendeleo ya mgonjwa Mwalimu Majid Sudi wakati huo maana yeye wakati Mwalimu anaumwa alikuwa London akihudhuria Jalsa ya U.K. na pia kushughulikia afya yake, hivyo aliporudi nilijikuta kuwa na jukumu la kumpa taarifa rasmi ya kifamilia juu ya afya ya Mwalimu Majid, hata kama ya kiofisi alipata kutoka kwa Maulana Sheikh Arif sahib, aliyekuwa anakaimu madaraka kwa kutokuwepo mkuu wakati huo.

Wakati Amir sahib akijibu maelekezo yangu yahusuyo mgonjwa Mwalimu Majid Sudi alitamka hivi; "Ni Mwalimu mchapa kazi na makini", alihuzunika sana sio huko tu alikopata taarifa ya ugonjwa wa Mwalimu, hali hiyo ilionekana zaidi pale pamoja na viwanja vya ripoti, mada na makala, hotuba za aina yake, ambavyo kila alyehusika kuwa na karibu na Mwalimu atakuwa na ya kusema lakini pia Mwalimu Majid Sudi alikuwa Mshairi, kwa mfano shairi lake la siku za hivi karibuni (aliloandika) alilotunga kuhusu Albino beti zake tatu zinasema:

Kuwaua Albino, dhambi ilokamilika
Kukata yao mikono, moyo unatetemeka
Mwache ufisadi uno, adhabu itatwepuka
Allah atakasirika, kawaua albino

Sikiza yao maneno, sana utaathirika
Kwikwi na kusaga meno, machozi yatiririka
Pinda kaunga mkono, nae yakabubujika
Tukomeshe kwa haraka, kuwaua albino
Kama tukisema 'No', damu haitamwagika
Tijara itakuwa 'No', wapi watavipeleka?
'No' ikija kuzaa 'No', amani taimarika
Kutakwisha tukitaka, kuwaua albino

Kwa neno zima Mapenzi ya Mungu ndio ushahidi tosha, hasa na wale wanaolisoma gazeti hili vyote hivyo, mada, makala, mashairi huchapwa mara kwa mara na gazeti hili juu ya usomaji, Mwalimu alipata nafasi ya kuongoza sala za Ijumaa maisha yake yote, hata hapa Dar es salaam na kule Kitonga kwenye mikutano yetu iitwayo Jalsa Salana, Mwalimu

Endelea uk. 5

Wasifu wa Mwalimu Majid Sudi Namwete

Kutoka uk. 4

wakati mwingine alipewa nafasi ya kusoma na hasa hotuba za mvuto za Makhalifa wetu, hivyo kipawa chake cha usomaji kilionekana wazi.

Juu ya ucheshi na ushauri kila mara alipenda kukaa katika vikundi vya mashauriano ya kihoja za kimahubiri na kama akina Mwalimu Abdul Imran sahib, Mwalimu Abdullah Mbanga sahib, kama hawa wanavyokuwa vinara katika vikao hivyo, bila kumsahau Mwalimu Mtamila.

Kutokana na hali hiyo ya ucheshi na ushauri aliposhindwa alikuwa hajisikii vizuri alikuwa mtu mwenye kumbukumbu kali, aliweza kukumbuka mambo mengi, madogo na makubwa hata ya zamani sana. Hali hiyo pia ilimfanya awe mwepesi wa kukumbuka hata "aya" wakati wa mahubiri na kuileta mahali pale na kumwacha mkadhibishaji akiwa na soni wazi wazi.

Hali yake inanikumbusha hali ya Mwalimu wetu mahiri Abdullah Mbanga yeye ana kipaji hiki sana, siku moja tukiwa Kunduchi Mtonani Kinondoni Dar miaka ile ya tisini tukifanya mhadhara pale, kama kawaida, imesomwa Qurani, na Mwalimu Fadhili Pazi, shairi, ikafuata mada mbili tatu, baada ya hapo ukaja wakati wa maswali na majibu - yale ya papo kwa papo. Ndipo akasimama sheikh mzee wa pale, baada ya kuona maswali, tangulizi yamejibiwa kama 'mboga' au 'staftahi' Bw. akaibuka na usomaji wa Kurani, aya fulani alizozitoa katikati ya Kurani, akasoma kidogo tu akaacha, kisha akakaa chini, ikawa hakueleweka, huku wengine tukijawa na hofu swali lile ni la mtindo gani? Aliulizwa (mzee) sheikh swali lako hapo ni nini? Alisimama na kusisitiza "ninataka uniambie aya hiyo inapatikana katika sura gani na juzuu gani na ina tafsiri gani? Kisha akakaa chini. (Huu siku zote kwangu nauita muujiza wa dhahiri, sijausahau). Ndipo Mwalimu Abdallah Mbanga alisimama na kumjibu yule sheikh, kwanza Mwalimu alisoma kile kipande, alichosoma yule shaeikh, ambacho sisi wengine tulisikia na kusahau pale pale, lakini Mbanga baada ya kukisoma kipande kile cha aya alimuuliza yule sheikh kuwa amekosea? sheikh akathibitisha kuwa hakukosea akakisoma nyuma yake zile aya zilizokuwa kabla na zile za baada yake bali lile fungu lote. Kisha akatafsiri neno kwa neno. Kitendo cha Mwalimu Mbanga kumaliza kutafsiri na kueleza ni sura gani na fungu la ngapi katika juzuu ile, sheikh na wapambe wake waliinuka na kuelekea kusikojulikana.



Mwl. Majid Sudi (waliosimama wa pili kutoka kushoto) pia hakuwa nyuma katika maswala ya michezo. ndani ya picha hii

Hiyo ndiyo hali ya waalimu wetu,kweli Allah Alhamdulillah Anawapa vitu adimu.

Alikuwa mwanamichezo na mpenzi:

Ijtimaa ya kila mwaka ambayo hufanyika Kitonga Ansarullah michezo huwa moja ya shamra shamra hizo za Ijtimaa. Kwa vile Malimu Majid Sudi ni mmoja wao, ameonekana kuwa ni mwanamichezo, yeye alikuwa anashiriki karibu kila mchezo yeye pamoja na rafiki yake maarufu Mwalimu Mustafa Mambo sahib ambaye ni mashuhuri katika Jamaat Ahmadiyya pia. Wao utakuta pengine wanafanya hata zoezi la ziada, huku Bw. Azizi Ng'amilo ambaye ni mwanamichezo mzoefu akiwa kocha wao ilimuradi onyesho fulani la furaha hutanda pindi walipokuwa wanaonekana kule kwenye viwanja vya Kitonga.

Nadhifu aliyetetea hadhi:

Mwalimu Majidi Sudi siku zote alikuwa nadhifu sawa na hadhi yake ya ualimu, ilimuweka kwenye chati alijitahidi sana kuitetea hali hiyo na kwa kweli amefuzu. maana wakati mwingine hali yake haikuwatofauti na masheikh wetu endapo ingekuwa humjui, kwa neno zima alikuwa mwalimu mzoefu hasa na hali hiyo aliijua na kuitetea. Alhamdulillah baadhi ya walimu sifa hizo wanazo. Kwa neno zima Mwalimu Majid Sudi alikuwa anaenda sawa na hali halisi ya mazingira na kujaribu kurahisisha kila linalotokea mbele yake kama "mcheza mpira" kuna jina la "kiraka" kila umwekapo anafaa.

Alikuwa si mwenye hisia za kujificha na alizibainisha mara moja hali hiyo, hata Amir aliyepita Bw. Ali Mosse aliwahi kuniuliza swali ambalo hadi leo sijasahau, aliuliza hivi, enzi za wadhifa wake, kwamba; "Hivi wewe na Mwalimu Majid ni ndugu rafiki, au ni ndugu tu?" Nilimwelewa na nilimjibu kuwa "Ah, kweli Mwalimu Majid ni ndugu na rafiki pia".

Mwalimu alionyesha hisia zake halisi na kufanikiwa kugusa mambo mengi kwa maneno machache, hapa utazingitia habari ya Allah, Jamaat, hata familia au ndugu na jamaa, hayo anayabainisha kupitia shairi alilotunga juu ya kifo cha marehemu baba Mzee Ahmad Sudi Namwete, anaandika hivi:

Msiba huu mzito, si peke umenifika
Dada walia kitoto, makaka wahangaika
Baba kaitika wito, tunapo pa kupashika?
Simba nimehamanika, baba kaitika wito

Nimefikia mkato, kwani shida kuandika
Tuchakate mchakato, auladiwe pulika
Tuyakamate kamato, memaye yalotukuka
Simba nimehamanika, baba kaitika wito

Pepo ipitayo moto, Jannat inosifika
Chonde liwe lake pato, mbele zako amefika
Ghaffuri mwenye mfuto, khatiaze kufunika
Simba nimehamanika, baba kaitika wito.

Mwalimu alikijua kifo chake mapema:

Miaka ya nyuma alinisisitiza kuwa mmoja wetu aombe kwa Amir akafanyie kazi mikoa ya karibu na Mdimba ili iwe rahisi kutoa ushauri kifamilia. Mimi nilimshauri yeye hasa yupo katika kukubalika zaidi, ushauri huo aliukubali ila utekelezaji ulikuwa bado, hizi ni enzi zile za Bw. Ali Saidi Mosse. Miezi ile ya mwisho ya 2010 alianza kunigeuzia kibao na kuanza kunihimiza mimi nifanye hivyo, hii ilisumbua sana kichwa changu kwa sababu ilikuja kinyume na makubaliano, nilifikiri kulikoni?

Mwanzo wa kuumwa kwake hadi umauti:

Wakati alipoanza kuumwa muda mfupi miezi ile ya Aprili - May 2011, mkewe Bi. Aminah binti Seif Hassan Nakuchima anasimulia kuwa aliota ndoto usiku "Wakiwa wamelala kitandani yeye na mumewe (marehemu) lilikuja jitu kubwa na refu likiwa limeshika silaha yenye ncha kali, kuona hivyo (yeye) ndani ya ndoto alipiga kelele, hata hivyo kelele hizo hazikusaidia, lenyewe liliwasogelea tu na kumtoboa toboa nacho Mwalimu kwenye macho na kumuacha akivuja damu, lenyewe hiloo likatokomea". Ndoto hii aliisimulia kwa Mwalimu mwenyewe! Yeye hakujibu neno. Mwezi Juni au Mei, hiyo hiyo Mwalimu alianza kuumwa malaria na homa , alipata tiba za kurudia zaidi ya mara tatu, magonjwa hayo yote mawili lakini hakukuwa na mabadiliko na nafuu. Ndipo katikati ya mwezi Juni alifika hapa Dar es salaam. Mara tu baada ya kufika alirudia ushauri wake kunisihi nifanye utaratibu wa kufanya kazi maeneo ya nyumbani.

Kama ndivyo basi, kabla hajaja hapa, habari zilifika Makao Makuu kuwa hali ya Mwalimu ni tete wakati huo kila mara alinijulisha kuwa hali ni tete! Tulishauriana na Sadr Ansarullah Taifa Bw. Inayatullah Seif Nakuchima, pia na makao makuu, wao makao makuu wakafikia muafaka Mwalimu aje hapa Dar es salaam kwa uchunguzi zaidi na vipimo zaidi, baada ya kushauriana na Jamaat ya Iringa Rais Bw. Rafiq na uongozi wote wa pale na wanajumuiyya akiwepo Mwalimu Abdullah Mbanga, baada ya jitihada kubwa walizozifanya na gharama za pesa na mali, walifikia muafaka wa kutafuta 'bakuri' m oja kali ambalo lilimsafirisha mgonjwa na mke wa marehemu na wasindikizaji wachache ambao walifika hapa Dar es salaam salimini. Makao Makuu wakiongozwa na Maulana Arif sahib, Katibu Mkuu Bw. Seif Hassan Nakuchima, Katib Mkuu mwenza Mwl. Abdulrahman M. Ame akina Mwalimu Omari Mnungu wakiwa na Sadr Ansarullah Taifa, Bw. Inayatulah Seif na wengine, tulikubaliana mgonjwa afike na aishi nyumbani kwa Sadr Ansarullah Taifa, naye Sadr alikubali jukumu hilo kwa moyo mkunjufu.

Baada ya kufika, mara moja alipelekwa Hospitali ya wilaya ya Ilala - Amana, kwa ushauri wa karibu wa Daktari wetu maarufu Dr. Kitabu Swaleh Pazi. Daktari pale Amana alimpokea na kufanya vipimo kwa kina, Daktari aligundua kuwa kumbe Mwalimu ana vidonda vya tumbo.

Alimpa tiba ya siku kadhaa, miezi ile nakumbuka ni kana kwamba watu wa makao makuu hawakuwa na kazi ingine bali kumsaidia Mwalimu tu, akina Mwalimu Ame, Nasri Matola, Mwalimu Ismail Mkoggas, Chikulupi Kawinga, akina Mwalimu Omari, Msesemele, walisimama imara kumsaidia bila kumsahau Bw. Jamilu A. Sudi Namwete ambaye ni mdogo wake marehemu.

Aliugua katika hali ya kuleta matumaini ya kupona, lakini huku yanaongezeka magonjwa, mara shinikizo la damu kushuka (Low Pressure), kuvimba miguu n.k Hali hii ilisababisha kufanya vipimo vya kurudia rudia katika hospitali mbalimbali hadi alipolazwa moja kwa moja katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili. siku 14 za mwisho kabla ya kifo chake Madaktari wakathibitisha kuwa kumbe tatizo hasa lilitokana na figo zote mbili kushindwa kufanya kazi. Hayo ndiyo maradhi yaliyosababisha umauti wa Mwalimu Majid Ahmad Sudi Namwete.

Aina fulani ya mahubiri:

Kule hospitalini Muhimbili ambako, ndugu, jamaa, rafiki na wapenzi wa aina mbalimbali walipishana kumjulia hali Mwalimu, bila kusahau Wanajumuiyya ambao walipofika waliacha athari maalum, maana wakifika baada ya kumuangalia mgonjwa wako au kabla huwa wanawajulia hali hata wagonjwa wengine ndipo wakati wanataka kuondoka walikuwa wanafanya maombi maalum bila shaka maombi yale yalikuwa mapana sana. Hii ilileta athari si tu kwa wagonjwa hata kwa Madaktari na waaguzi.

Wakati ule mimi na mdogo wangu Bw. Abdallah Rashidi Kumonellah, tulifanya zamu ya kushinda pale, kutoa huduma ipasavyo kwa mgonjwa wetu, yeye mchana mimi usiku, tulijikuta tunalazimika kupiga deki vyooni mara kwa mara, kwa sababu ya kujaa maji machafu mara kwa mara. Hali hiyo ya deki na usafi iliwaathiri sana wagonjwa na Madaktari - baadhi yao walitupenda sana hata mmoja alidiriki kusema "Kwa kweli sio tu mnamsaidia mgonjwa wenu tu bali wagonjwa wa wodi nzima". Bila shaka hawakupenda kuondoka kwetu.

Hali ya mwisho ya Mwalimu ilikuwa hawezi kujimudu, jitihada iliyofanywa ya kuwa karibu nae (hapa ikumbukwe ni utaratibu wa hospitali hususan Muhimbili hawataki mtu mwingine pale zaidi ya mgonjwa tu). Ushirikiano ulioonyeshwa kati ya mke mkukbwa Bi. Amina Seif na wifi yake, Mama Rukiyya ambaye ni mke mdogo wa marehemu, mimi na mdogo

Endelea uk. 9

Bustani ya Washairi

SIMBA DUME UMEKWENDA

1. Inalillahi tamko, natamka nikikonda,
Chozi la mtiririko, kuzuia lanishinda,
Yamekufika mauko, sahibu nilokupenda,
Simba dume umekwenda, pokewa vyema mbinguni.

2. Nalia kwa huzuniko, unyonge umenitanda,
Nahisi mwingi mchoko, moyo kasi wanienda,
Ila sina lalamiko, kazi ya Mola Mtenda,
Simba dume umekwenda, pokewa vyema mbinguni.

3. Akhi kumbukumbu lako, kichwani limeniganda,
Wema na ukimya wako, na moyo usio inda,
Kisha taadhima yako, kwa wakongwe na makinda,
Simba dume umekwenda, pokewa vyema mbinguni.

4. Namisi makala zako, zenye lugha tafsida,
Na hoja zenye miweko, tulivu zisizopinda,
Zilowanyima vicheko, adui wenye husuda,
Samba dume umekwenda, pokea vyema mbinguni.

5. Usimba lakabu yako, ni kweli uliiranda,
Katika yetu misako, ulikubuhu kuwinda,
Na hukuwa simba koko, bingwa wa kurandaranda
Simba dume umekwenda, pokewa vyema mbinguni.

6. Utii, umakiniko, kwenye chati ulipanda,
Hukuwa na nung'uniko, hata walipokuponda,
Si mwana malalamiko, wewe ni mwana mkenda
Simba dume umekwenda, pokewa vyema mbinguni.

7. Manju mwenye fasihiko, na beti zenye mawanda,
Metupa mfadhaiko, wadau wa hii kada,
Tunakosa burudiko, la kiada na ziada,
Simba dume umekwenda, pokewa vyema mbinguni.

8. Ulijasiri kivyako, kueneza Tauhida,
Ukahimili vituko, vya kila ulikokwenda,
Hata mahasimu wako, hukiri kwa ushuhuda,
Simba dume umekwenda, pokewa vyema mbinguni.

9. Uliamsha chereko, hata katika kandanda,
Mido wa michachariko, wa kushuka na kupanda,
Aghalabu timu yako, ilikuwa ikishinda.
Simba dume umekwenda, pokewa vyema mbinguni.

10. Kwa mengi masikitiko, nakuaga Sudi nenda,
Nitaiga kwa mashiko, mema uliyoyatenda,
Nakuombea limbuko, peponi unakokwenda,
Simba dume umekwenda, pokewa vyema mbinguni.

Mwl. Abdallah Khamis Mbanga (Kungwi)
S.L.P 359 Iringa

SIMBA DUME KATUTOKA

1 Msiba uliotuka, umetokea mapema
Habari zimetufika, yahuzunika mitima
Majidi ametutoka, duniani amehama
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

2 Simba dume katutoka, hatunalo la kusema
Ndivyo alivyoandika, Muumbaji alo mwema
Duniani katoweka, si pakudumu daima
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

3 Haya ninayotamka, roho inanisukuma
Mapenzi aliyoweka, Mwalimu ninomsema
Ji muhali kutoweka, bali yabaki salama
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

4 Ali mshauri wangu, mambo yalipopindama
Tumtegemee Mungu, Tuombe kwa taadhima
Wamekiri na wenzangu, nasaha zake ni njema
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

5 Mwalimu Majidi Sudi, Mola umlaze pema
Twakuomba kwa juhudi, tusikileze Karima
Umlipe kwa juhudi, ya matendo yake mema
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

6 Mwalimu mstaarabu, alijaliwa hekima
Ajapo kutuhututubu, twaongezeka elimu
Kamtunuku Wahabu, tabia yake ni njema
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

7 Mkufunzi wa Jamia, kwa kazi alijituma
Mhubiri wa mikoa, ni bingwa wa taaluma
Al-malidi wajua, simba wa kitaaluma
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

8 Wao wanaelezea, sababu wao kuzama
Pindi wakimzomea, Majidi hutabasama
Majibu nayangojea, mmemaliza kuzoma?
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

9 Muandishi wa makala, aziondowe shutuma
Wasomapo lahaulla, maadui wanakwama
Alitimiza dhamira, kuuelimisha umma
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

10 Ali-mhadhiri bora, jalsa ikiandama
Yu mhutubu imara, hutufunza ya Karima
Hutuba zake ibura, Mola Umpe rehema
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

11 Simba alimshairi, ni pigo kwa taaluma
Kaondoka askari, mlinzi wa isilama
Ona yake mashairi, yalivyojaa hekima
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

12 Simba wa Ahmadia, Masihi wetu wa zama
Safina aliingia, amefariki salama
Kufa hujambeua, ndicho kifo cha heshima
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

13 Yafaa kujiandaa, sisi tulo baki nyuma
Masurufu kuyatwaa, ona siku za yoyoma

Mauti yana sogea, twatoka zamu kwa zamu
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

14 Mola dua ipokee, jalia Waisilama
Vipaji utuinue, tukutumikie vema
Na Majidi mpokee, Muweke mahali pema
Karejea kwa Karima, simba dume katutoka

Mwl. Mubaraka A. Nyamihasi
S.L.P 391 Tarime - Mara

ALAZWE PEMA

1. Tulizipata habari, toka watu na majini,
Maradhi mengi hatari, yamemshika mwilini,
Ilikuwa ni safari, kuondoka duniani,
Alazwe pema peponi, kwa heri babu kwa heri.

2. Si sote ni wasafiri, tuendao kwa manani
Erabi Mola kahari, usie chako kifani
Twakuomba mghafiri, na adha za kaburini
Alazwe pema peponi, kwa heri babu kwa heri.

3. Kila nikitafakari, ninajawa na huzuni,
Masomo mengi mazuri, alitufunza chuoni,
Kwa hoja za mahubiri, ni nyingi alibaini,
Alazwe pema peponi, kwa heri babu kwa heri.

4. Alikuwa askari, mpiganaji makini,
Vipaji alishamiri, kutoka kwa Rahman,
Na tungo za mashairi, Simba dume kwenye fani,
Alazwe pema peponi, kwa heri babu kwa heri.

5. Alitujuza fasiri, ya kitabu cha Qur'an,
Aya za fumbo na siri, alichambua undani,
Hekima na ujasiri, akatujenga yakini,
Alazwe pema peponi, kwa heri babu kwaheri.

6. Uadilifu nakiri, alikuwa namba wani
Hakua mwenye kiburi, eti dongo la kusini
Aliona ni fahari, kupenda wote moyoni
Alazwe pema peponi, kwa heri babu kwa heri.

7. Alikuwa ni mzuri, mithiri ya bustani
Alinukia uturi, kwa kupenda yake dini
Alikuwa mwenye ari, kufundisha darasani
Alazwe pema peponi, kwa heri babu kwa heri.

8. Tunakuombea heri, makazi mema mbinguni
Yaghafuru yaghafuri, tudhaifu insani
Mwepushie kila shari, msamehe ya ayuni
Alazwe pema peponi, kwa heri babu kwa heri.

9. Beti tisa nakariri, dunia sio thamani.
Tukae kwa tahadhari, tujiandae jamani
Emola utusitiri, mwishoe iwe amani.
Alazwe pema peponi, kwa heri babu kwaheri.

Mwl. Najab Fakim Said
Mafisa Kilindi - Tanga

TWAOMBA UTUKIDHIE -EWE MOLA MAUJUDI

1 Bisimillahi Wadudi, kwa jinalo nianzie
Mbele yako nasujudu, Allah nikuhimidie
Ninainuwa aidi, yatata tutatulie
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

2 Mwaka mpya uwe mudi, thamani tuthamanie
Mambo yetu yawe udi, yote utufukizie
Tusawazishie hadi, sawasawa tutulie
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

3 Naomba kitajuwidi, kwa heshima na ushue
Ewe Mungu Musfadi, rehema utushushie
Baraka bila idadi, nazo utupezo sie
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

4 Ya Allah ya Maujudi, Wewe Watujuwa sie

Ni wa dhaifu zaidi, hatuna siha afie
Utupe afya shadidi, viwiliwili vijae
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

5 Iwande yetu jasadi, homa homa uwaondoe
Maradhi yasituzidi, hadi kitako tukae
Siye pia auladi, tupe siha na rahae
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

6 Tupe moyo na fuadi, swafi tukutumikie
Jana, leo hadi ghadi, njia utuangazie
Nguvu tupate zaidi, uchovu usiingie
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

7 Mwaka uwe zumaridi, tuwe afu tunukie
Tubaki kama waridi, mauwa yatupepee
Tuwe watu wa juhudi, ya dini tusisinzie
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

8 Tusifanye ukaidi, batwili sikumbatie
Wala tusiwe abidi, Jalali tukukatae
Tuwepo wa kujirudi, maovu yasituvae
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

9 Allah, tusiwe baidi, ibada tuendelee
Mno swala ikibidi, kamwe tusiiachie
Tubaki nayo abadi, hadi kifo kifikie
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

10 Na kisha utusaadi, riziki tuzidishie
Tutakapo taradadi, tufungulie tujae
Tupate yanayobidi, neema utujazie
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

11 Utukunjulie sudi, kipato turuzukie
Cha halali utufidi, tafadhali tujalie
Na shukurani tuzidi, Weye tukushukurie
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

12 Yetu yaende spidi, juu yasining'inie
Walakini ikibidi, baraka yamiminie
Nasi tutajitahidi, kwako tukukurubie
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

Endelea uk. 7

Kutoka uk. 6

13 Utulinde na hasidi, ubaya awaniae
Niaye na makusudi, vivunjwe kama vigae
Tukusanyie junudi, sisi watusaidie
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

14 Tulinde tusiritadi, ibilisi azugae
Yake yasiwe miradi, tukanasa tunasue
Allah, nyuma tusirudi, shetani kando akae
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

15 Nakhitimu kuradidi, nchi yetu ibakie
Ibaki ilimuradi, kitali utufutie
Na isalie biladi, salama tujikalie
Twaomba utukidhie, Ewe Mola Maujudi.

Al-Ustadh Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala rangi tatu
Dar es Salaam.

KAMA WATAKA KUTUNGA

1 Sanaa za maandiko, shairi tunazotunga
Kwa kweli zina miiko, yake tunapoyaenga
Tunga uwe na kumbuko, usije haribu kunga
Kama mwataka kutuna, kutunga kuna miiko

2 Tungo zinazo miiko, mnaopenda kutunga
Mjuwe za miinuko, na mabonde ya kuwinga
Myatowe ya mnyoko, na ya kutasa wakunga
Kama mwataka kutunga, kutunga kuna miiko

3 Pawepo mtiririko, wa maneno kuyapanga
Msarifu kwa mapiko, msanifu kwa kujenga
Watu waweke kitako, kwa lugha njema kubonga
Kama mwataka kutuna, kutunga kuna miiko

4 Mfahamu maandiko, na sheria ya kutunga
Kanuni, muwala viko, vina, mizani za kunga
Urari uwe tandiko, silale kwenye michanga
Kama mwataka kutuna, kutunga kuna miiko

Al-Ustadh Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala rangi tatu
Dar es salaam.

DHIHAKA

1 Alo na meno makali, kinywani tele mzingo
Wala hana mushikili, kuzitafuna finyango
Na hana shida kwa kweli, kuibangua mihogo
Si dhihaka si mipango, unasimama ukweli

2 Mtazame wa mapengo, anapotoa kauli
Anasema kwa maringo, mate yasije kwa feli
Mate katika mapengo, hutawanya vindawili
Unasimama ukweli, si dhihaka si mpango

3 Haoni vyema sabili, mtu aliye na chongo
Hata ende sipitali, hawatoi tongo tongo
Basi ukumbuke hili, elimu ina kiwango
Si dhihaka si mpango, unasimama ukweli

4 Mchaji hana maringo, hanati na hajidhili
Kweli mbali na uwongo, na jengo japo kamili
Haishi bila mlango, kwa kila mwenye akili
Si dhihaka si mipango, unasimama ukweli

Al-Ustadh Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala rangi tatu
Dar es salaam.

LEO SI SAWA NA JANA - MAMBO YAMEBADILIKA

1 Bisimillahi ni jina, la Allah Mola Rabuka
Nalo hili kama shina, hubeba yenye baraka
Nakuzowesha kijana, na wewe kulitamka
Mambo yamebadilika, ya leo siyo ya jana

2 Ninasema huu mwaka, uliopita wa jana
Wa elimu ya hakika, hutathimini mapana
Wapi walitetereka, kosa wasifanye tena
Ya leo siyo ya jana, mambo yamebadilika

3 Kwangu niliyoyaona, napenda kuyaandika
Yasomeni waungwana, yasomeni mkitaka
Bali kubwa la maana, tukae tukikumbuka
Mambo yamebadilika, ya leo siyo ya jana

4 Mambo yamebadilika, ya leo siyo ya jana
Watu tumeongezeka, sana tumezaliyana
Na wengi wametoweka, na sisi wameachana
Ya leo siyo ya jana, mambo yamebadilika

5 Yamebadilika sana, ya zamani yanatoka
Tena yale ya maana, ya maadili hakika
Yanatuka ya laana, ya madhambi na shabuka
Mambo yamebadilika, ya leo siyo ya jana

6 Mno yamebadilika, watu kama hayawana
Kutenda na kutamka, wala khilafu hakuna
Twafauti kuumbika, khulka tumelingana
Ya leo siyo ya jana, mambo yamebadilika

7 Kabisa tumelingana, kwa twabia twajivika
Twafika kutafunana, mithili panya na paka
Wengine tunamezana, kama samaki twadaka
Mambo yamebadilika, ya leo siyo ya jana

8 Na tumeparang'anyika, japo watu twajazana
Dunia ni kama nyika, utu taabu kuona
Hata biladi ya Makka, hali ni hii Madina
Ya leo siyo ya jana, mambo yamebadilika

9 ALlahuma Maulana, utuongoze twarika
Ambayo kona haina, ile iliyonyooka
Ile ya Masayidina, na mitume watukuka
Mambo yamebadilika, ya leo siyo ya jana

Al-Ustadh Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala rangi tatu
Dar es salaam.

UVIVU HAUPENDEZI

1 Mwenyezi Mungu Azizi, Mwenye uwezo na nguvu
Nipe ari nibarizi, khabari bai angavu
Wakumbuke wakumbuzi, kuna Aduwi uvivu
Haupendezi uvivu, uvivu haupendezi

2 Tujibidiishe kazi, tuifanye kwa wagivu
Masika na kiangazi, tujiweke washupavu
Za ofisi na palizi, biashara na uvuvi
Haupendezi uvivu, uvivu haupendezi

3 Uvivu haupendezi, hangaika kama ndovu
Tushughulike kwa kazi, tuupate uzowevu
Natufanye mapinduzi, kuuondoa uvivu
Haupendezi uvivu, uvivu haupendezi

4 Tusiidharau kazi, ya halali na wokovu
Dhambini haitwingizi, yenye malipo yang'ivu
Mungu bariki tajazi, Atatupatia mbivu
Haupendezi uvivu, uvivu haupendezi

5 Tusiifanye ajizi, tutumie yetu nguvu
Ya akili na ujuzi, kwa elimu na kwa wivu
Wivu wa maendelezi, kwa juhudi na utuvu
Haupendezi uvivu, uvivu haupendezi

6 Acheni ya uchafuzi, enyi vijana welevu
Chukuwa khabari hizi, ganja lina upumbavu
Pia latia uchizi, wazimu na ulegevu
Haupendezi uvivu, uvivu haupendezi

7 Kabisa haupendezi, twabaki watepetevu
Hutufanya wadowezi, na kuomba kwa mabavu
Haitupasi wazazi, wala wana wasikivu
Haupendezi uvivu, uvivu haupendezi

8 Tama ya masimulizi, siyo swahiba uvivu
Uvivu king'ang'anizi, ni ndugu yake uchovu
Uchovu ni ulegezi, si wenye ukakamavu
Haupendezi uvivu, uvivu haupendezi

Al-Ustadh Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala rangi tatu
Dar es salaam.

TUKIOMBEE SHUFAA - KIZAZI CHETU CHA LEO

1 Bisimillahi Manani, Ndiye Muumbaji Bwana
Wa ardhi na mbingu, wa usiku na mchana
Jua na mwezi vindani, mwa Himayaye Rabana
Tukiombee shufaa, kizazi chetu cha leo

2 Ninataka kuwapeni, maelezo waungwana
Malezi angalieni, kizazi chenu kubana
Kila mara jaribuni, maadili kufunzana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

3 Sawa sawa yatunzeni, maadili mema yana
Fadhila na stahani, na kwa imani hufana
Tuyape hayo thamani, tuyaheshimu bayana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

4 Tulipo pawalakini, kila mmoja aona
Kila pande duniani, uchafu umejazana
Basi tujitahidini, sana kuelimishana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

5 Kizazi kipya jamani, ki mbali na subhana
Ki mbali mno na dini, na dini wameachana
Wengi wao wakindani, hata Allah wamkana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

6 Enyi wazazi oneni, oneni hali ya wana
Wapo kama hayawani, kwa vitendo na kunena
Ni watu bali manyani, usoni haya hawana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

7 Maadili hatuoni, kufatwa na hawa wana
Twabiya za uzunguni, waiga kwa nguvu sana
Zetu za uswahilini, huona hazina mana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

8 Wawe wao ni misheni, ya dini yao hawana
Hawaendi kanisani, kumuomba Maulana
Hao na wao shetwani, wote wakubaliyana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

9 Na kwa wale waumini, wa Islam salana
Hawendi Misikitini, kumuabudu Rabana
Washinda madanguroni, kwa usiku na mchana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

10 Oneni Mabaniyani, Singasinga walingana
Ni nani mwenye imani, kati yao mnaona?
Hawaendi hekaluni, mungu wao watafuna
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

11 Kizazi kipya katwani, madili mema hakina
Kimezama kilindini, kwenye dhambi warandana
Juhudi tuifanyeni, tuwarejeshe vijana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

12 Ah! hebu tazameni, waoneni hawa wana
Wabugiao kokeni, na kwa bangi wajichana
Na madawa ya ureni, wayanywa kwa kuchuwana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

13 Mashoga wamesheheni, ni wengi wamejazana
Wanatoga sikioni, hereni wanavishana
Na shanga za kiunoni, na mikufu wapeyana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

14 Wasichana maskini, visa vyao ninaguna
Wanajivisha vimini, na mavazi ya kubana
Piya libasi laini, na chupi zaonekana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

15 Wazazi changamkeni, wana wetu waowana
Hebu ya Lutwi someni, nini kilipatikana?
Kemeeni, kemeeni, hiyo ni kubwa laana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

16 Wafanya hayo jirani, wao nasi twakutana
Wanaketi majumbani, tuishimo twaonana
Si wageni asilani, mabinti na wetu wana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

17 Ni mkubwa mtihani, Alotupa Maulana
Vizuri tuufanyeni, na tena kwa kushindana
Tuombe kwake Manani, kwa swala na zaidana
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

18 Nimefika kituoni, Mola wangu Sayidina
Tumenasa tuauni, Tunasuwe kinamna
Sivyo, tumo khatiyani, muokozi nani tena?
Tukiombee shuffaa, kizazi chetu cha leo

Al-Ustadh Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala rangi tatu
Dar es salaam.

"Mwelewe Maulvi Nuruddin"

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. na kutafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Jamil Rahman Rafiq

Kutoka toleo lililopita

MAWAIDHA YA MWISHO

Sheikh Rahmatullah r.a. wa Lahore aliahidiwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwamba yeye ataweka msingi wa jengo lake alilonuia kulijenga mjini Lahore, lakini Masihi Aliyeahidiwa a.s. akafariki mapema. Mnamo juni 1912, Sheikh Rahmatullah r.a. akamwomba Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. kutimiza ahadi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s., naye akakubali mara moja. Akaenda Lahore tarehe 15 Juni na jioni hiyo akaweka msingi baada ya kutoa hotuba fupi ambamo alisema:

"Mpendwa wangu na mfadhili wangu alimwahidi Sheikh Sahib kwamba ataweka msingi wa jengo lake kwa mkono wake mwenyewe, lakini mpango wa Mungu ulikuwa ya kwamba ahadi hiyo itimizwe na mtumishi wake mmoja. Bwana Sheikh akaniandikia nifike kwa shughuli hii. Sina afya nzuri, naumwa sehemu kadha za mwili, lakini nina shauku ya kutimiza ahadi ya bwana wangu mpendwa.

Majengo mengi yamejengwa na yanajengwa pembeni mwa kiwanja hiki, lakini sisi twalipenda hili jengo litakalojengwa kwa sababu ya kibinafsi na ya Kijumuiya. Upendo wa kibinafsi ni kwamba marehemu Hadhrat Mirza Sahib a.s. aliahidi kuweka msingi wake, na kwamba ahadi hii itatimizwa na mtumishi wake. Upendo wa Kijumuiya ni kwamba Jumuiya yetu pia ina sehemu yake katika jengo hili. Wanajumuiya wapaswa kuomba kwa bidii kwamba matokeo yake yawe mema na wakazi wa jengo hili na waliosimamia wawe wema na wapende mema.

Nimesema ya kwamba Jumuiya nzima inahusiana na jengo hili: Natumai nyinyi nyote mtaomba kwa bidii kwamba Mungu Alibariki na kwamba wazao wa Bwana Sheikh anayetupenda nao watupende kama apendavyo yeye. Sasa nitaliweka tofali moja la msingi kwa maombi, na kisha Sahibzada Mirza Mahmud Ahmad, Bashir Ahmad, Sharif Ahmad na Nawab Muhammad Ali Khan, kila mmoja wao aweke tofali moja moja kwa maombi."

Tangu safari yake ya kwenda kutembelea Lahore hapo kabla, msikiti ulikwisha jengwa tayari katika "Ahmadiyya Buildings." Hivyo tarehe 15 Juni alipowasili tu Lahore akaelekea msikitini, akasali rakaa mbili na akaomba kwa bidii sana kwa wale waliochukua jukumu la kuujenga msikiti na kwa wazao wao. Kesho yake akauhutubia mkusanyiko mkubwa wa wanajumuiya. Katika hotuba yake alisema:

"Mungu Mtukufu amewakusanyeni baada ya Mtume Mtukufu s.a.w. kwa njia ya mfalme wetu, Masihi Aliyeahidiwa a.s., na baada ya kufariki kwake Akawahifadhini kwa mikono yangu msifarakane. Thaminini ukarimu huu wa Mungu ipasavyo, wala msijiingize katika mabishano na dhana mbaya. Siwezi kuwaza faida ipi ya kikhulka au ya kiroho mnapata kutokana na mabishano hayo. Mungu Mwenyezi Amemfanya *Khalifa* yule Aliyempenda na Akawafanyeni kumtii yeye. Ni ujinga wao tu wanaolaumu kazi ya Mungu. Nimewaambieni mara kwa mara na kuwaonyesheni kutoka katika Kurani Tukufu ya kwamba si kazi ya binadamu kumfanya mtu yeyote kuwa *Khalifa*. Ni Mungu tu Anayefanya *Makhalifa*. Nani alimfanya Adamu kuwa *Khalifa*? Mungu Akasema: Mimi Nitamweka *Khalifa* katika ardhi (2:31). Malaika wakapinga: Ataleta uharibifu ardhini na kumwaga damu. Lakini ukinzani huu ukawafaa nini? Mwaweza kusoma ndani ya Kurani Tukufu kwamba mwishowe wakalazimika kutii. Kama mmoja wenu ananitoa kosa, na hata kama yu malaika, nitamwambia: Yafaa uutii *Ukhalifa* wa Adam. Na akikataa kwa kiburi na kushika kazi ya *Iblisi*, hapo akumbuke kumpinga Adamu kulimfaa nini *Iblisi*. Nakariri ya kwamba mtu hata kama ana tabia ya kimalaika akipinga *Ukhalifa* wangu, tabia yake njema itamwongoza kumtii Adam; lakini kama yu *Iblisi*, ataiondoka jamii hii tukufu.

Daudi a.s. alikuwa *Khalifa* mwingine, kama ilivyonenwa: Ewe Daudi, hakika Tumekujaalia kuwa *Khalifa* ardhini (38:27). Yeye naye alifanywa *Khalifa* na Mungu. Wapinzani wake walikuwa wachochezi wa fitina dhidi ya utawala wake, ambao baadhi yao walipata kuingia katika ngome yake; lakini nani awezaye kufaulu katika kumpinga yule aliyefanywa *Khalifa* na Mungu?

Kisha Mungu Mwenye Enzi Akawafanya Abu Bakr r.a. na Umar r.a. kuwa *Makhalifa*, Mungu Awaridhie wote hao wawili. *Marafidhii* (Washia) hadi sasa wanapiga kelele na kulia kwa nini walipata *Ukhalifa*. Lakini hamwoni kwamba mamilioni ya Waislamu wanawaombea baraka Abu Bakr r.a. na Umar r.a. Wallahi mimi nami nimefanywa *Khalifa* na Mungu. Msikiti huu umenipendeza moyo wangu. Nimewaombea kwa bidii wale wote ambao waliuchangia ujenzi wake kwa njia yoyote, nami nina yakini kwamba maombi yangu yamefikia Arshi. Nikiisha wasili mjini humu na nikisimama katika msikiti huu ulionipendeza, natangaza kwamba jinsi Mungu Alivyowafanya Adamu, Daudi, Abu Bakr na Umar kuwa



Maulana Hadhrat Hakeem Nuruddin
Khalifatul Masih I r.a.

Makhalifa, ndivyo Alivyonifanya mimi kuwa *Khalifa*.

Kama mtu akisema *Anjuman* imenifanya *Khalifa*, ataongopa. Fikira kama hizi zaleta maangamio; jihadharini nazo. Sikilizeni sana mara nyingine, hakuna mtu wala *Anjuman* iliyonifanya *Khalifa*; sioni *Anjuman* yoyote ina uwezo wa kumfanya mtu yeyote kuwa *Khalifa*. Hakuna *Anjuman* yoyote iliyonifanya *Khalifa*, wala sithamini kabisa *Anjuman* kufanya hivyo. Sijali katu *Anjuman* yoyote kutengana nami. Hamna mtu awezaye kuninyang'anya joho hili.

Katika fikara yao, nani alistahili kuwa *Khalifa*? Kuna Mahmud nimpendaye ambaye ndiye mwanaye mpenzi wangu na mfadhili wangu. Tena kuna Nawab Muhammad Ali Khan r.a. aliyemwoa bintiye, na mkewe Mir Nasir Nawab r.a., na mkewe Ummul Muminina r.a. Hao tu ndio pekee wanaoweza kufikiriwa kwamba wanadai *Ukhalifa*. Ni la ajabu ya kwamba wale wanaodhani kuwa haki ya hao imenyang'anywa hawazingatii kwamba hao wote ni watii waaminifu kwangu. Hawakupeleka madai yao mbele ya wakinzani. Warithi wa Hadhrat Mirza Sahib a.s. na jamaa zake wa karibu, wote hao ni waaminifu kwangu. Nawaambieni kweli kwamba kati yenu hakuna hata mmoja anitiiye kama watiivyo wapenzi wangu Mahmud, Bashir, na Sharif, tena Mir Nasir Nawab na Nawab Muhammad Ali Khan. Sisemi hivyo ili kuwafurahisha, bali naieleza kweli ilivyo kwamba wananipenda kwa kutaka wapate radhi ya Mungu. Nimepata kusikia Ummul Muminina akihakikisha mara ma-ishirini kwamba yeye anajifikiria kuwa mtumishi wangu. Mian Mahmud yu mtu mzima; atawaambieni kwamba ananitii kwa uaminifu. Mkinzani aweza kusema kwamba huyo si mwaminifu kwangu katika kunitii; lakini nina hakika kabisa kwamba yu mtii kwangu kwa uaminifu zaidi sana kuliko yeyote kati yenu. Ahali zake Hadhrat Mirza Sahib a.s., wananitii wote kama vile Ali r.a., Fatima r.a. na Abbas r.a. walivyomtii Abu Bakr r.a., bali zaidi. Kila mmoja wao ni mwaminifu sana hata kwamba siwezi kuwaza ya kuwa yeyote kati yao aweza kunidhania vibaya.

Sikilizeni, abadan sikuwa na uchu wa kuwa *Khalifa*. Nilivyovaakablasijawamfuasiwa Hadhrat Mirza Sahib a.s., ndivyo ninavyovaa hivi leo. Nimewahi kuishi kati ya waheshimiwa na watawala kwa heshima nami nikavaa hivyo hivyo. Baada ya kuwa mwanafunzi wa Hadhrat Mirza Sahib a.s. sikugeuza mtindo wangu wa maisha. Baada ya yeye kutuacha mkono, Mungu Akafanya Alivyopenda. Hata sikupata kuwaza kwamba nitakuwa *Khalifa*, lakini Mungu kwa hekima Yake Akapenda na kunifanya Imam na *Khalifa* wenu, na wale mnaowafikiria wanastahiki kupata *Ukhalifa* Akawafanya wanitii. Sasa m nani kubisha? Kama hamna budi kutafuta kosa, basi nendeni mkamtafutie Mungu kosa, lakini jihadharini na adhabu kwa kufanya ufidhuli huu na utovu wa adabu. Simsifu yeyote isivyostahili, sipendi hata nisalimiwe na mtu yeyote. Sihitaji sadaka zenu na riziki yenu. Mungu Anilinde nisiwaze hata kuipata. Mungu Mweza Amenijaalia hazina zilizofichikana ambazo hakuna mtu wala kiumbe anayezijua. Mke wangu na watoto wangu hawamtegemei yeyote kati yenu. Mungu Anawapatia. Mwaweza kumpa nini mtu yeyote. Mungu yu Mkwasi; nyinyi ni mafakiri (47:39)

Aliyepo hapa asikilize vizuri na kuwafikishia wasiokuwapo ya kuwa wazo hili kwamba waliostahiki *Ukhalifa* wamenyimwa ni wazo la *Marafidhii* (Mashia), na lazima liepukwe. Mungu Mweza Amemfanya kwa mkono wake *Khalifa* Aliyemwona anastahiki kupata *Ukhaifa*. Ampingaye yu mkosefu na mwasi. Muwe malaika na kujitoa na kutii; msiwe kama *Iblisi*. Kuzusha kwenu swala la *Ukhalifa* ni *Urafidhii* (Ushia). Basi pelekeni malalamiko yenu mbele ya Mungu kwamba mkazi wa Bhera amekuwa *Khalifa*. Tena kuna wengine wasemao: *Khalifa* anafanya nini? Baadhi yao wasema: Yeye anawasomesha tu vijana. Wengine wanasema: Yu msomi, na saa zote anashughulikia vitabu tu. Mwaweza kunitoa mokosa elfu; kunitoa kwenu makosa kutakuwa kumpinga Mungu Aliyenifanya *Khalifa*. Hao watafuta makosa ni kama *Marafidhii* (Mashia) wanaoendelea kuwatafutia makosa Abu Bakr r.a. Umar r.a.

Swala jingine mnalohitilafiana juu yake ni: Tuwafikirije wapinzani wetu? Sikilizeni sasa vyema. Neno la Mungu limekwisha fafanua kawaida kuhusu kumkubali Nabii na kumkataa. Wakati wowote nabii adhihiripo kunakuwa hakuna mushkili katika kupambanua wanaomwamini na wamkataao. Achilia mbali elimu ya kupambanua mema na mabaya, Mwenyezi Mungu Amekwisha weka kanuni kuhusu kutoamini, kuamini na kufanya ushirikina. Manabii wamepita zamani. Kila mara walipatikana walioamini na waliokataa. Je, mna shaka kuhusu habari hii; na je, mliona mushkili muwapange katika kundi gani wale wasiowaamini hao manabii?

Mwaambiwa kanuni za imani na ukosefu wa imani. Hadhrat Mirza Sahib a.s. alikuwa Mjumbe wa Mungu. Kama asingelijiita Nabii, angelifanya kosa la kuikataa Hadithi ya Mtume s.a.w. iliyomo katika kitabu cha *Muslim* ambamo ameitwa yule ajaye kuwa Nabii. Swala la kumwamini au kumkataa lipo wazi. Kama yule amkanaye ajiita Mwislamu, yeye mtu huyo yupo karibu nanyi jinsi Wakristo walivyo karibu nanyi kuliko Wayahudi. Kadhalika Waislamu wanaomkataa Hadhrat Mirza Sahib a.s. waweza kuwa karibu nasi kuliko watu wengine. Yule amwaminiye Hadhrat Mirza Sahib r.a. lakini anikataa mimi ni kama *Warafidhii* (Washia) wanowakataa masahaba wa Mtume Mtukufu s.a.w. Jambo liko wazi sana, lakini wasio na shughuli nyingine wanajishughulisha katika ukinzani usiofaa.

Tena baadhi ya marafiki zangu wanasema kwamba wanajumuiya wa Lahore wanapinga *Ukhalifa*. Nimewahi kutaali Kurani Tukufu na Hadithi kwa waalimu, nami naziamini kwa uaminifu. Moyo wangu umejaa mapenzi ya Kurani na Hadithi. Nimetumia maelfu ya rupia kwa kujinunulia vitabu vya maisha ya Mtume s.a.w. na historia ya Islam. Mtaala wote huo umehakikisha imani yangu ya kwamba hakuna awezaye kuzuia kitu Anachonuia Mungu kukifanya. Nimetaja kwamba Adam a.s. na Daudi a.s. walikuwa *Makhalifa* na nimeeleza Abu Bakr r.a. na Umar r.a. walikuwa *Makahalifa*. Aidha, nimewaambieni kwamba jinsi Abu Bakr r.a. na Umar r.a. walivyo *Makhalifa*, ndivyo Mungu Alivyonifanya kuwa *Khalifa* baada ya Hadhrat Mirza Sahib a.s. Lakini hapa kuna habari zaidi kidogo. Mungu Amesema: Kisha Tukawafanyeni *Makhalifa* ardhini (10:15). Nyinyi nanyi mlifanywa *Makhalifa* katika ardhi, japo huo ni *Ukhalifa* wa aina nyingine. Basi, ni Mungu pekee Anayefanya *Makhalifa* wala hakuna awezaya kumzuia Yeye.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Habari Katika Picha





(Picha ya juu) Katika kusherehekea mwaka wa 50 wa uhuru wa Tanzania Bara Jumuiya ilionesha mchango wake kwa vitabu ilivyochapisha.

(Picha ya chini yake) Akili hukaa kwenye mwili ulio na afya. Michezo inapewa kipaumbele katika Jumuiya.





(Picha ya juu) Bwana Abdillah Kombo akitoa maelezo ya mchango wa Jumuiya ya Ahmadiyya katika uhuru wa Tanzania bara

(Picha ya chini yake) Picha ya magazeti ya zamani ya Mapenzi ya Mungu yakielezea mapambano ya uhuru.

Wasifu wa Mwalimu Majid

Kutoka uk. 5

wangu Abdallah, hadi marehemu anafariki bila kumuacha peke yake, wale madaktari walisikika wakitoa pongezi kwa kusema "wengi huwaacha wagonjwa wao wakifa peke yao, bali wanakabidhi na kuwatelekeza, wakifa wanaanza kuuliza uliza ilhali wao ndio wenye mgonjwa wao, kwa kweli poleni, lakini pia tunawapa pongezi".

Mwalimu Majidi alifariki tarehe 23/11/2011 saa 4:30 asubuhi siku ya Jumatano na alizikwa Alhamisi tarehe 24/11/2011 saa kumi na moja jioni. Mara baada ya kifo chake, nilianza kutoa taarifa ya kifo chake kwa njia ya simu kwa kumpa taarifa Bw. Inayatullah Seif - Sadr Ansarullah Taifa ili pia atoe taarifa kwa Amir sahib. Kama ilivyo kuwa wakati wa kuumwa kwake ndugu na jamaa walitoa pole nchi nzima, Masheikh na Walimu ndugu na jamaa, wengine baada ya kupewa rukhsa na Amir sahib bali alitangaza kila anayeweza afike kwenye mazishi, nakumbuka Masheikh kadhaa na Walimu walifika mazishini, kwa mfano akina Sheikh Yusuf A. Kambaulaya, Sheikh Ahmad Daud Mmoto, Sheikh Bakri Abedi na wengineo, Walimu akina Mwalimu Adamu wa Ifakara, Mwalimu Abdullah Mbanga kutoka Iringa na wengineo waliwawakilisha Masheikh na Walimu wachache ambao hawakufika.

Shukurani:

Hapa ninaomba nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa ndugu, marafiki na Waaminio, bali Makao Makuu dar es salaam, Jamaat ya Iringa kwa ujumla ambao wamefanya kila liwezekanalo katika kuokoa maisha ya Mwalimu Majidi Sudi, lakini mapenzi ya Allah siku zote ndiyo yanapewa kipaumbele.

Amir sahib ambaye alikosa raha siku zote kwa ajili ya kipenzi chake, Masadr, Sadri Ansarullah Taifa naye amefanya na kuahidi kufanya kila liwezekanalo, Madaktari wakiongozwa na Dr. Kitabu Pazi, hawa na wengineo ambao kila mmoja ni shahidi kwa lile alilolifanya kwamba kwa kweli alifanya kwa kupata radhi ya Allahtu.

Mwisho; Kwako Mhariri wa Mapenzi ya Mungu - Mahmood Hamsin Mubiru kwa kunipa moyo, bali kunishauri kuwa niandike wasifu wa Mwalimu wetu mpenzi. Nakumbuka siku ile ulipofika pale Muhimbili na kumuona mgonjwa (marehemu) ulishtuka kuona hali ya uvimbe wa miguu ya Mwalimu, kwa kweli hukukaa tena pale bali uliondoka kumtafuta Dr. Kitabu Pazi afanye lolote juu ya hali ile.

Basi ndugu zanguni, kama ilivyoagizwa na Allah Karim na kunukuliwa na Mwalimu mwenyewe kuwa; "Hakika ardhi ni ya Allah, Atairithisha Amtakaye katika watumishi Wake, na mwisho mwema ni kwa Wamchao" (Qurani Tukufu sura 7:129).

Mwisho



Picha za Viongozi wa Jumuiya wakikutana na viongozi wa nchi na taasisi mbalimbali duniani.

Leo ni Dr. Zainabu Saidi Mkinde

Kutoka uk. 12

Kutokana na gharama kubwa za ada pale St. Anthony, kulikuwapo majadiliano ya kifamilia kuhusu hilo. Aende Jangwani Sekondari au aendelee pale pale St. Anthony ambapo hadi wakati huo keshakata mwezi mmoja tayari. Wazazi wa Zainabu waliamua aende Jangwani Sekondari kufuatiana na gharama ya ada kuwa ndogo ambayo wangeweza kumudu kulipa.

Aingiwa na wasiwasi

Kutokana na mabadiliko hayo ya shule, Zainabu alikuwa na wasiwasi sana kwani katika kipindi kile kifupi alikwisha zowea mazingira ya St. Anthony. Alikuwa hahitaji nauli ya shule. Lakini sasa kwa sababu ya kwenda Jangwani itabidi nauli. Alikuwa anawahurumia wazazi wake mzigo wanaojitwisha. Zainabu alilidhihirisha hilo kwa wazazi wake. Mwisho wa yote ikakubalika Zainabu kuhama kutoka St. Anthony hadi Jangwani.

Zainabu aliniambia kuwa alipoanza masomo yake ya sekondari Jangwani, kidato cha kwanza hakufanya vizuri sana kutokana na mabadiliko ya shule yaliyofanyika. Anasema kulikuwa na tofauti kubwa ya mazingira. Mazingira ya shule za binafsi yalikuwa bora zaidi kwake na kwamba huko haupo kabisa upungufu wa waalimu. Waalimu wapo wa kutosheleza. Hapakuwa kipindi chochote kilichokosa mfundishaji.

Matatizo ya usafiri

Zainabu alinieleza kwamba aliathirika sana juu ya usafiri wa kutoka Mbagala hadi Jangwani Sekondari. Watoto wa shule huwa hawajaliwi na wenye mabasi. Mara kadhaa hakujaaliwa kuwahi vile vipindi vya kwanza pale asubuhi. Mwanzoni uhaba wa vitabu, maabara na maktaba pale Jangwani pia vilichangia kwa sehemu kubwa asifanye vyema.

Ssasa masomo yakolea:

Zainabu aliendelea kuniambia kwamba alipoingia kidato cha pili mambo yaligeuka. Alianza kutenda vizuri sana katika masomo yake. Hali hiyo ilijiri baada ya yeye kufanya jitihada ya makusudi katika kujisomea na kufanya mazungumzo na wanafunzi wenzie mbalimbali. "Na khasa", Zainabu alikazia usemi wake, "pale nilipomtegemea sana Mwenyezi Mungu, masomo yangu niliona mepesi mno".



Dr. Zainabu Saidi Mkinde mara baada ya kutunukiwa shahada ya udaktari akiwa kwenye vazi maalum kwa ajili ya tunuku hiyo

Kadhalika Zainabu aliniambia kwamba akiwa shuleni alikutana na wanafunzi wenye khulka na tabia mbalimbali Kwa kweli kulikuwa na mtihani wa namna ya watu kuishi pamoja. Basi, Zainabu akasema kuna wale wanafunzi ambao walikuwa wanapenda shule na wengine wao fikira na mawazo yao hayakuwapo shuleni. Hawa walielekeza mambo yao kwenye starehe na anasa. "Kwa bahati njema, mimi kwa ajili ya malezi mema ya dini ya Kiislam chini ya Jumuiyya ya Ahmadiyya, yalinisaidia mno kuepuka vishawishi vya vikundi mbalimbali vibaya. Rafiki zangu mimi walikuwa wale waliokuwa wanapenda masomo". Zainabu alieleza hayo wakati nikimsaili juu ya mambo mbalimbali.

Kila alipokuwa anasonga mbele, Zainabu uelewa wake kwenye masomo ulikuwa mzuri sana. Mara zote alikuwa anapeleka mambo yake ya masomo na mengine kwa Mwenyezi Mungu. Mwenyewe anasema huo ndio msingi mkubwa wa mafanikio yake.

Kwa namna hii, Zainabu alifaulu vizuri mitihani ya taifa ya kidato cha nne kwa kupata daraja la kwanza. Alifanya vizuri sana juu ya masomo ya Kemia na Baolojia na alipata alama ya 'A'.

Ajiunga Kilakala:

Mnamo mwaka 2004, Zainabu alijiunga na shule ya wasichana wenye kipaji maalumu kule Kilakala Sekondari - Morogoro. Alikuwa kule hadi mwaka 2006 alipokhitimisha masomo yake. Hapo alichukuwa masomo ya 'PCB' -yaani Fizikia, Kemia na Baolojia na alifaulu vizuri sana kwa kupata daraja la kwanza.

Chuo cha utabibu:

Baada ya kufaulu vizuri katika masomo yake hayo, mnamo mwaka huo huo wa 2006, Zainabu alichaguliwa kujiunga na chuo kikuu kishiriki cha Tiba cha Muhimbili. Achilia mbali uchaguzi huo wa chuo, lakini Zainabu nilipozungumza naye aliniambia kwamba fani ya udaktari tangu alipokuwa madarasa ya chini alikuwa anaipenda na ndiyo sababu alihamia kwenye masomo ya sayansi 'PCB' ili aweze kusomea utabibu.

Naam, sasa Zainabu anaanza masomo ya udaktari. Anayazamia mbizi. Basi katika kipindi hicho mambo mengi ya kutisha yalijitokeza. Kwa kweli ule mwaka wa kwanza, masomo aliyaona magumu mno kwake. Aliniambia alipata wastani mchache ambao hajawahi kupata tangu aanze shule. Hali hii ilimstua sana Zainabu na kumkatisha tamaa. Aliniambia alitaka kubadilisha fani hii na kuingia nyingine kwa kuhisi fani ya udaktari hataimudu. Lakini kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, alipata washauri wema waliompa matumaini na moyo wa kuendelea mbele na mchakato wake wa kuchukua fani ya udaktari. Alisema ushauri wa wazazi wake, ushauri wa Dr. Mmoto na ushauri wa Dadaye Dr. Tausi Maftah, ulitosha kumsimamisha imara Zainabu katika hili. Akaendelea na masomo yake ya udaktari.

Aingiwa woga:

Zainabu aliniambia pia kwamba alipoamua kufanya kila juhudi katika masomo na kumwomba sana Mwenyezi Mungu, mambo aliona yanaenda barabara. Aliendelea kufanya vizuri sana na kukuza matumaini yake.

Aliniambia Zainabu kwamba alipokuwa kwenye chumba cha kujifunzia masomo ya upasuaji na kuangalia miili ya watu waliokufa alipata khofu na wasiwasi mwingi mno. Kwa maneno yake mwenyewe, Zainabu alitamka; "hivyo mwanzoni mwa mafunzo hayo nilikuwa nakwepa sana kwenda katika chumba cha upasuaji (Theatre), lakini baadaye nilizowea". Mambo yakawa kama kawaida.

Zainabu Mkinde masomo yake ya udaktari yamechukua miaka mitano na kutunukiwa shahada ya kwanza baada ya kufaulu vizuri. Sasa anaitwa Dr. Zainabu Saidi Mkinde.

Nilimuuliza ana lengo gani la baadaye, Dr. Zainabu alijibu na kusema kwamba atafanya kazi na serikali miaka michache ijayo. Mwelekeo wake anataka kuwa Daktari bingwa.

Dr. Zainabu anawashauri mabinti wa Ki-Ahmadiyya wajitahidi sana na wafanye bidii sana kwenye masomo yao. Wamwombe na wamtegemee sana Allah ili Awafanyie wepesi katika masomo yao. Aliniambia kwamba kwenye mashule na vyuo vipo vishawishi vingi khasa kwa mabinti, kwa hiyo alitaka mabinti wa Kiahmadiyya washike barabara maadili ya Kiislam. Alisema hiyo ni dawa tosha ya kumuwinga shetani.

Wazazi wamshukuru Mungu:

Wazazi wa Dr. Zainabu wametoneka sana na hatua aliyofikia binti yao huyu. Wamefurahi, tena wamefurahi sana. Walitayarisha dhifa maalumu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumfikisha binti yao hapa alipo. Dhifa hiyo ilifanyika tarehe 17/12/2011 nyumbani kwa Bwana Saidi Mkinde kule Mbagala. Watu kadhaa walialikwa na kuhudhuria. Watu takribani 150 walishiriki kwenye sherehe ya dhifa hiyo. Shughuli ilianza baada ya sala ya Adhuhuri kwa usomaji wa Kurani Tukufu iliyosomwa na Mwalimu Yusufu Mwishehe kisha Mwalimu Mohamedi Namwete alisoma shairi lililotungwa na Lajna wa kanda ya Mbagala. Baadaye mwenyeji wa dhifa hiyo, Bwana Saidi Mkinde aliwakaribisha wageni wake wote na akataka wajione kama wapo nyumbani na washirikiane naye katika shukurani hiyo kwa Allah.

Kulikuwepo mada mbili muhimu zikihusiana khasa na tukio hilo. Mada ya kwanza ilikuwa juu ya umuhimu wa elimu katika Islam. Mada hii ilizungumzwa na Sheikh wa Mkoa wa Dar es salaam Maulana Waseem Ahmad Khan. Yeye alielezea umuhimu mkubwa uliofundishwa na Islam katika kutafuta elimu, si ya dini tu, bali ya kila aina.

Mada ya pili ilikuwa juu ya Uislam, Heshima na haki ya wanawake. Mada hii ilizungumzwa na Mwalumu Abdulrahman M. Ame kwa urefu kabisa. Aliwaambia wasikilizaji wake kwamba Uislam haukuwafanya wanawake wawe watu wa mekoni tu, bali wamepewa fursa ya kutafuta elimu na kufanya kazi kwa kuvaa mavazi ya kujistiri. Mwanamke kujistiri ni heshima wala si wivu. Mwalimu Ame aliwaasa wale akina mama wanaochangamkia mavazi na unaodhaniwa ustaarabu wa kisasa, kuvaa nguo fupi na kwenda mgongo nje si maendeleo bali ni maradhi ya nafsi, wanawake wa Kiislam wakatae kuambukizwa nao.

Kwa niaba ya ndugu na jamaa, palikuwapo khutuba mbili. Moja ilitolewa na Sadr Khuddamul Ahmadiyya na ya pili ilitolewa na Sheikh Waziri kwa niaba ya majirani.

Mwisho Dr. Zainabu Saidi Mkinde aliwashukuru sana wazazi wake wote wawili kwa kumsomesha na kumpa moyo na kufikia alipofikia. Aliwataka Wanajumuiyya kusomesha watoto wao bila kujali jinsia. Alisema bila elimu tutakuwa tumekwisha. Tumechelewa mno wenzetu wale wametutangulia. Dr. Zainabu anataka kuona Waahmadiyya wanakuwapo katika kila fani. Hii ni kwa ajili ya maendeleo ya Jumuiyya.

Naam, hadi sasa kwa fadhili za Mwenyezi Mungu kwenye fani ya udaktari tunao mabinti wawili. Wa kwanza ni Dr. Tausi Maftah na leo tumepata wa pili Dr. Zainabu Saidi Mkinde. Mwenyezi Mungu tunamuomba hawa wote wawili waje kuwa maprofesa, Amina thuma Amin.

Uonevu chanzo cha makundi ya kigaidi

Kutoka uk. 12

kuwa ulimwengu wa Kiislamu leo hii umedhoofishwa si tu na mgawanyiko wa makundi mbalimbali bali pia kuhasimiana miongoni mwao. Ni jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya pekee ndio inaweza kutembea kifua mbele na kudai kwamba imeungana, katika umoja ambao unatokana na mfumo uliopo wa Ukhalifa.

Khalifa Mtukufu a.t.b.a aliwakumbusha wasikilizaji kuwa mustakbali mwema wa binadamu leo hii umewekwa rehani kutokana na husuda. Sera za kikatili na uonevu sanjari na matendo ya nchi zenye nguvu ndio yanachochea makundi ya msimamo mkali na ugaidi. Sambamba na hilo, Khalifa Mtukufu a.t.b.a alisema:

"Amani ya kweli na haki ya kweli haviwezi kupatikana kokote duniani leo hii. Badala yake matamanio ya kidunia yamekithiri na kuvuka mipaka. Watu pamoja na Serikali zinautazama utajiri na mali za watu wengine kwa jicho la husuda. Leo hii serikali duniani zinadai kwamba zinapigania ili kutafuta amani na kuwaokoa raia dhidi ya uonevu. Madai haya ni ya udanganyifu kabisa na ulaghai. Malengo ya serikali hizi ni kutimiza maslahi yao binafsi na kupora utajiri wa mataifa mengine. Hivyo, kwa kisingizio cha kutafuta haki, damu za watu humwagika na matokeo ya uonevu na dhuluma hiyo ni kuibuka kwa makundi mengi ya kigaidi."

Kiongozi huyo wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya pia alitumia fursa hiyo kuonya dhidi ya makundi yote yenye msimamo mkali. Alisema kwamba makundi yote yenye msimamo mkali yanatakiwa kukomeshwa, vinginevyo, yatasababisha hatari kubwa.

Akizungumzia hususan nchi ya India, alisema kwamba ingawaje nchi hiyo inadai kuwa haina uhusiano wa kidini, baadhi ya Waislamu wenye msimamo mkali tayari wamejipenyeza nchini humo na matendo yao yanasababisha madhara kwa jamii. Alisema kwamba makundi hayo tayari yamelenga kuwashambulia Waislamu Ahmadiyya walioko nchini humo na kwamba makundi hayo yenye msimamo mkali yamekuwa yakijaribu kuishawishi Serikali ya nchi hiyo izuie shughuli za amani na za kibinadamu zinazofanywa na Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya nchini humo.

Akielezea kuhusu upinzani huo, Khalifa Mtukufu a.t.b.a alisema:

"Kamwe na daima Waislamu Ahmadiyya hawataacha kumwabudu Mungu Mmoja na kufuata mafundisho ya Mtume Mtukufu s.a.w. Hata hivyo, nawaambia wale wanaoamini katika haki na usawa kwamba kama mnayakubali makundi yenye msimamo mkali kwa ajili ya manufaa ya kisiasa basi fahamuni kwamba hapana shaka yoyote nchi yenu itatumbukia katika mapigano. Kama mtaruhusu makundi haya kuenea hayatasababisha chochote bali kuporomoka kwa maadili."

Khalifa Mtukufu a.t.b.a alimalizia kwa kusema kuwa matumaini yapo, na matumaini hayo yamejikita katika mafundisho ya Mtume Mtukufu S.a.w ambayo ni amani, udugu na upendo. Katika kutimiza shabaha hii, Mtume Mtukufu S.a.w alijitolea muhanga katika muda wote wa maisha yake. Aidha, katika zama hizi, ni Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya ambayo inaendelea kufuata nyayo zake. Hivyo, Khalifa Mtukufu a.t.b.a alisema kuwa Waislamu Waahmadiyya wote ni lazima waelewe majukumu yao.

Khalifa Mtukufu a.t.b.a alisema:

"Je, inatosha tu kwa sisi kujiita Waislamu Ahmadiyya? Je, hili litatosha kuleta amani duniani? Hapana! Ili kuleta amani ni lazima kwanza tuelewe tabu ambayo Mtume Mtukufu s.a.w alihisi kwa ajili ya binadamu wote. Kila matendo yetu na kila juhudi yetu inatakiwa iwe kwa ajili ya kumaliza ukatili wote. Ili kuleta haki ya kweli, lazima tufanye jihadi dhidi ya ukatili. Jihadi yetu haifanywi kwa kutumia silaha yoyote bali kwa njia ya maombi kwa binadamu wote. Hii ndio njia pekee ya kuleta amani na upendo katika jamii;" alisisitiza kiongozi wa waaminio.

Matumizi mema ya kipaji

Kutoka uk. 12

Waswahili husema Wasitara hasumbuki wambili havai moja. Mwenendo huu wa mauaji ya Albino ulimgusa sana Simba dume na kwa majozi makubwa alilia:-

Kuwauwa Albino, dhambi

iliyokamilika,
Kukata yao mikono, moyo unatetemeka,
Mwache ufisadi uno, adhabu itatuhepuka,
Allah atakasirika, kuwauwa Albino,

Sikiza yao maneno, sana utakasirika,
Kwikwi na kusaga meno, machozi yatiririka,
Pinda kaunga mkono, naye yakabubujika,
Tukomeshe kwa haraka, kuwaua Albino.

Ulimwengu wa Kiislamu kwa hivi sasa umo katika mashaka makubwa. Hakuna umoja wala maelewano. Tunaonekana dhaifu na wasiojiweza. Nini hasa chimbuko la udhaifu wetu?. Simba dume anajibu na anasema Ukhalifa ndio dawa mjalabati kwa maendeleo ya Uislamu.
Ni zawadi kubwa na sote tunatakiwa kuipokea . Kuhusu hili Simba dume anasema:-

Kuukana ni msiba, ukhalifa kwetu neema,
Neema ilo matwilaba, gizani ndiyo najima,
Najima tena ni twiba, pulikeni enyi umma,
Kuukana ni msiba, Ukhalifa kwetu Neema.

Misiba katika maisha ni jambo la lazima na linamkomaza mja na kilele cha msiba ni kifo. Kifo kwa binadamu ni wajibu na habaki mtu mmoja katika safari hiyo. Hapana shaka kifo huacha kovu na haya ndiyo yaliyomkuta Simba dume alipofiwa na baba mzazi.

Huzuni iliyomzito, msiba ulonifika,
Kweli dunia mapito, ili sijaghafirika,
Moyo wapwita mpwito, wangu baba kunitoka,

Mwl. Abdulrahman Ame kwa haraka alimpa pole Simba dume na kumwambia :
Pole kwa chako kilio, simba dume baba yangu,
Hilo ndilo ishilio, la kwako wewe na kwangu,
subira na vumilio, ndiyo dawa ya machungu,
Sisi sote ni wa Mungu
Kwake ndio marejeo.

Ubeti huu wa Mwalimu Ame unanikumbusha ubeti alioandika Sheikh Kaluta Amri Abedi akimpa pole Bahran Ulumi Mahmood Hamduni Jitu kali alipofiwa na baba yake alimtuliza na kuimba
Pole bin Hamduni, kufa pia ni rehema,
Tungedumu duniani pasi kufa na kuhama,
Tungekuwa mashakani kwani dunia si njema,
huna baba huna mama uwe na Mola daima.

Hapana shaka malipo ya ihsani ni ihsani. Mwalimu Suleiman Jailani Likoko alifanya kazi kubwa ya mahubiri huko kusini. Mzee Namwete alijiunga kutokana na jitihada hiyo ya Suleiman. Hakuna zawadi kubwa unayoweza kupewa kama kuonyeshwa njia ya kumfikia Masihi aliyeahidiwa a.s. Simba dume alikumbuka ihsan hiyo ya Suleiman na alipofariki hakujizuia kuomboleza.

Ni kilio cha huzuni, mzee wetu likoko
Suleimani Jailani, kisha tangulia huko
Kenda kwa wake Manani, katuachia huzuniko
Mpe jema pumziko, ya Azizi Rahman

Mahubiri yanahitaji hekima,

busara, ucheshi na khulka njema. Na hizi ndizo sifa alizokuwa nazo Simba Dume katika mahubiri. Alitaka utamaduni huu uigwe na wengine na hivyo akausia:-

Waadhi pulikeni, dini muisambazao
Ili amani iwini, kusiwe na mao mao
Ndipo uwe furahani, kafiri na waabuduo
Kusiwe na mao mao, sote twataka amani

Maisha ya Simba dume ni kioo kwetu. Yapo mambo tunaweza kujifunza, kwa mathalani kuvitumia vyema vipaji tulivyopewa na Mwenyezi Mungu kwa faida ya wengine. Ni jambo ambalo amejitahidi sana Simba dume. Kipaji chake cha ushairi alikitumia vyema kwa manufaa ya binadamu. Yatapatikana maendeleo makubwa iwapo kila aliyepewa kipaji na Mwenyezi Mungu akijitahidi kutumia kipaji hicho ili kiweze kuwanufaisha binadamu. Kwa ujumla maisha yetu yote ikiwa ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu basi tutapata radhi ile ambayo inatupa ukaribu na Mwenyezi Mungu. Na tutaokoka tukizingatia kanuni hii.

"Sema: Hakika Sala yangu, na sadaka yangu, na uzima wangu, na kufa kwangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mwumba wa walimwengu". (6:163)

TANGAZO KUTOKA KITENGO CHA UTAFITI WA VITABU RABWAH PAKISTAN

Kitengo cha Utafiti wa vitabu kilichopo Rabwah Pakistan kinapenda kuwatangazia wanajumuiya wote kwamba kitengo hicho kimepewa jukumu la kuandaa orodha kuu "Master Catalogue" ya vitabu vyote vya Jumuiya na vile vilivyoandikwa na Wanajumuiya.
Hivyo Mwanajumuiya yeyote aliyewahi kuandika au kuchapisha kitachu cha aina yoyote kwa jina lake kuanzia mwaka 1889, anaombwa apeleke taarifa hizo kwenye kitengo hicho ili kitabu chake kiweze kuingizwa kwenye orodha hiyo kuu.
Taarifa zinazotakiwa kutumwa ni:
Jina la kitabu, Mwandishi/Mfasiri, Toleo, mahala kilipochapishwa, tarehe ya uchapishaji, Mchapishaji, idadi ya kurasa, ISBN, Lugha na Maudhui.
Aidha mwanajumuiya yeyote aliye na kitabu chochote cha Jumuiya cha zamani naye anaombwa awasiliane na kitengo hicho.
Tafadhali wasiliana nao kwa:

Incharge Research cell, P. O. Box #14 Chenab Nagar (Rabwah), Pakistan
Ph. 0092476214953,
Mob: 3344290902
Fax: 0092476211943
Email: research.cell@saapk.org

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

Mapenzi ya Mungu

Rabi' ul-awwal 1433 AH | Januari 2012 | Sulh 1390 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Ayyub bin Mussa r.a. kutoka kwa baba yake kisha kwa babu yake ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema. Hakuna baba aliyempa mwanaye zawadi bora kuliko adabu njema, yaani ulezi bora (*Tirmidh*)

Kiongozi wa Ahmadiyya duniani aweka bayana:

Uonevu chanzo cha makundi ya kigaidi

Aonya makundi yenye msimamo mkali kuwa ni hatari

Na Jamil Mwanga, Dar es Salaam

Imeelezwa kuwa majanga yanayotokea katika maeneo mbalimbali duniani ikiwemo uharibifu unaosababishwa na makundi ya kigaidi, unatokana na hali iliyokithiri ya kutoweka kwa haki na usawa miongoni mwa jamii.

Hayo yamesemwa hivi karibuni na Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani, Khalifa Mtukufu a.t.b.a, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a alipokuwa akitoa hotuba ya kufunga Mkutano wa Mwaka uliofanyika Qadian, India. Kiongozi huyo alikuwa akihutubia kutoka msikiti wa Baitul Futuh, London ambapo hotuba hiyo pia ilirushwa moja kwa moja kwa njia ya satelaiti. Waumini zaidi ya 17,000 kutoka maeneo mbalimbali duniani walihudhuria mkutano huo huko Qadian huku wengine zaidi ya 4,000 wakikusanyika katika msikiti wa Baitul Futuh, London kusikiliza hotuba ya Kiongozi wa waaminio iliyokuwa nzuri na ya kusisimua.

Khalifa Mtukufu a.t.b.a alisema kuwa kutokana na uonevu uliokithiri na kutoweka kwa usawa katika jamii, hali ambayo inatafsiriwa kuwa ndio wakati muafaka kwa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya kote duniani kushika hatamu ya kuwaongoza watu kuelekea katika njia ya uadilifu na haki.

"Leo hii ni jukumu la kila Muislamu Ahmadiyya kuilinda dunia dhidi ya uharibifu. Hii ni kwa sababu tumefanya Ba'iat na kuungana na Masihi Aliyeahidiwa (amani iwe juu yake) na kwa kufanya hivyo, tumeapa kwamba daima tutajitahidi kwa ajili ya mustakbali mwema wa binadamu wote.", alisema.

Kiongozi huyo Mtukufu a.t.b.a aliendelea kusema

Endelea uk. 10



Masjid Baitul Futuh London.
Kutoka Msikiti huu - ambao ni wa kwanza kwa ukubwa barani Ulaya - Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. aliuhutubia moja kwa moja kupitia kituo cha MTA mkutano wa mwaka wa 112 Qadian India.

Leo ni Dr. Zainabu Saidi Mkinde

Na Mwandishi wetu maalum

Dr. Zainabu Saidi Mkinde mwezi Desemba mwaka 2011 amefuzu katika fani ya utabibu na kuwa Daktari wa binadamu, Alhamdulillah. Masomo hayo amechukuwa chuo kikuu kishiriki cha Tiba cha Muhimbili cha jijini Dar es salaam. Ametunukiwa shahada ya kwanza ya udaktari baada ya masomo yake ya miaka mitano katika chuo hicho.

"Haikuwa kazi rahisi kwangu khasa ukizingatia ugumu uliopo wa masomo ya udaktari, lakini kwa msaada wa Allah nimefika hapa nilipofika hivi sasa" alinieleza wakati nikizungumza naye.

Katokea wapi?

Zainabu Saidi Mkinde alizaliwa mwaka 1986 Temeke jijini Dar es salaam. Ni mtoto wa kwanza wa Bwana Saidi Mkinde na Bi. Rehema Makungu. Zainabu alianza masomo ya shule ya msingi mnamo mwaka 1993, kwenye shule ya msingi Mbagala kizuiwiani. Mwenyewe anasimulia; "Kutoka darasa la kwanza hadi la nne uwezo wangu wa masomo ulikuwa wa kawaida hadi nilipofikia darasa la tano, nilipoanza kufanya vizuri zaidi hadi darasa la saba ambapo nilifaulu vizuri, nikachaguliwa kujiunga na shule ya wasichana ya Jangwani hapa jijini Dar es salaam.

Hamu na shauku ya kupenda kusoma

Zainabu kabla hajapata matokeo ya mtihani wake wa darasa la saba kwa kuwa yalichelewa kutolewa, hakukaa tu kimya, bali alianza masomo ya kidato cha kwanza katika shule ya St. Anthony Mbagala ambako alisoma kwa muda wa mwezi mmoja tu. Hii ilitokana na uchu wa kutafuta elimu. Yeye aliona kusubiri na kukaa bure tu haingefaa bila kubukua. Matokeo ya mtihani yalipotolewa na wizara ya Elimu, Zainabu akawa amechaguliwa kwenda shule ya Sekondari ya Jangwani.

Endelea uk. 10

Matumizi mema ya kipaji

Na wa Mamba

Mwalimu Majid Sudi Ahmad Namwete kwa lakabu ya ushairi 'Simba Dume' alikuwa mshairi aliyetumia sanaa hii ili kumsaidia binadamu amaizi kusudio la kuumbwa ambalo ni kuabudu na kutimiza wajibu kwa Muumba na viumbe wake. Hakuna kilichomsumbua kama kufikisha ujumbe wa Masihi aliyehaidiwa as. Maudhui katika mashairi yake yalitawaliwa na dhamira hiyo na hivyo kufanya mashairi kuwa sehemu ya mahubiri.

Mtukufu Mtume Muhammad saw alisema "kwa hakika katika ushairi kuna hekima" haitokuchukua muda kutambua kuwa Simba dume amesadifu vilivyo maneno ya bwana wa mabwana Mtukufu wa daraja, mbora wa Manabii Hadhrat Mustafa Muhammad saw. Kama tulivyokwisha sema kalamu ya Simba dume daima ililenga katika kumkumbusha binadamu sababu ya kuumbwa kwake.

Sanaa ya ushairi kwa Simba dume ilikuwa ni mbinu nyingine ya kufikisha ujumbe wa Masihi aliyeahidiwa. Sanaa hii aliipa mwelekeo na akasisitiza kama alivyosisitiza mwaandishi maarufu wa Urusi Niko Layevich Tolstoy kuwa mwandishi anawajibu wa kumtanabaisha mwanadamu juu ya tope lililotanda katika dunia yetu hii na kumuokoa ambaye kwa bahati mbaya amekwisha zama katika tope hizo.



Mwl. Majid Sudi (enzi za uhai wake) akitoa hotuba katika Mkutano wa mwaka - Jalsa Salana, 2011 Kitonga Dar es Salaam

Nia ikiwa ni kumnusuru kiumbe huyo ili nafsi yake isafishwe na kuwa nyeupe mithili ya theluji kwenye mlima Kilimanjaro. Kila shairi alilolitoa Simba dume lilizingatia muwala, vina, mizani na maudhui ya msingi ikiwa ni kueleza yakuwa wagonjwa wote waje kwa haraka kwani tabibu wa kweli wa kututibu maradhi yetu amekwisha dhihiri katika dhati ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian a.s. Kila shairi lake ukilisoma unafaidi utamu wa sanaa na kukuonyesha njia iliyonyooka.

Dini kwa Simba dume ilikuwa na maana pana yaani kuwatumikia binadamu kwake ilikuwa ni sehemu ya dini. Maonevu kwa binadamu ni jambo ambalo ni baya kwa kila anayemuhofu Mola wake.

Simba dume alikerwa na kusikitishwa sana na ukatili uliochanganyika na ujinga kwa wale wanaodhani ya kwamba utajiri unapatikana kwa kutumia viungo vya Albino. Ujinga uliofurutu ada! Kama Mola hajakupa hujapata.

Endelea uk. 10